Nipashe
Jumatano Aprili 29, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580218
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



TOLEO MAALUMU

## Tamwa yamuenzi Dk. Mengi kwa usawa na haki za binadamu

UKURASA 3


14 siasa

Trump 'alivyoichefua dunia' kukata msaada kwa WHO

Uingereza haina mpango wowote kusitisha ufadhili wake kwa WHO yenye wajibu mkubwa kuongoza dunia katika masuala ya afya

UKURASA 14

# Mbaroni wakiuza sukari bei ya juu

• **Ni** kutokana na operesheni iliyoendeshwa kuwasaka waliokaidi bei elekezi, wafungiwa maduka, wasambazaji wakubwa waonywa... *Endelea Ukurasa 2*



**BAA LA CORONA**

**Kwa kuwa baadhi ya watu walioambukizwa hawawezi kuonyesha dalili za ugonjwa wa Covid – 19, inashauriwa kila mara kuacha nafasi kati ya mtu na mtu kwenye eneo ambalo ugonjwa huo umesambaa. WHO**
- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## Wagonjwa wa corona Zanzibar sasa 105

UKURASA 2



## Jaji Augustino Ramadhani atakavyokumbukwa

UKURASA 2


Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

**MICHEZO** **FIFA YAITAKA TFF KUTUMIA 'SAB' 5** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6




Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd (kulia), akipokea hundi ya mfano ya Sh. milioni 30, kutoka kwa Meneja wa Benki ya NMB tawi la Zanzibar, Abdalla Duchi, ikiwa ni msaada wa kukabiliana na mapambano ya maradhi ya corona (Covid-19). Makabidhiano hayo yalifanyika ofisini kwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar,Vuga jijini Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara mbaroni kisa kuuza sukari bei juu

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WAFANYABIASHARA saba wamekamatwa katika wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro na maduka yao kufungwa baada ya kubainika kupuuza amri ya serikali ya kuuza sukari kwa bei elekezi ya Sh. 2,700 kwa kilo moja na kuendelea kulangua kwa bei ya Sh. 3,500 kwa kilo.

Pia wafanyabiashara wakubwa wawili wanaosambaza sukari kwa bei ya jumla wilayani humo, wameonywa baada ya kubainika kufanya ulanguzi wa bidhaa hiyo, huku serikali ikiahidi kufanya uchunguzi zaidi baada ya stakabadhi za kielektroniki za mauzo yao kuonyesha bei ya ulanguzi, hata baada ya tangazo la serikali.

Jana, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, akiwa ameongozana na maofisa wa Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Mapato (TRA), Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) na maofisa biashara wa wilaya hiyo, walifanya operesheni ya kushtukiza katika maduka makubwa tisa na kubaini kupuuzwa kwa maelekezo ya ukomo wa juu wa bei ya sukari.

"Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alishatoa maelekezo kuhusu sukari na wiki iliyopita Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alitangaza bei elekezi ya sukari kwa kila mkoa. Ninyi bado hadi leo (jana) mnauza kilo moja kwa Sh. 3,500, tena wakati huu wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

"Wananchi wenzenu maskini mnawauzia, tena bila huruma sukari kwa bei ya ulanguzi ya Sh. 3,500, yaani tuteseke kwa corona, tuteseke kwa mafuriko ya mvua na wakati huohuo tuwatese wenzetu Waislamu walioko kwenye funga ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Hapana na haiwezekani!

"Ofisa Biashara, funga hayo maduka yote mpaka nitakapotoa maelekezo mengine na OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya) kamata hao wafanyabiashara wakahojiwe kwa kukaidi amri ya serikali," Ole Sabaya aliagiza.

Mkuu wa Wilaya huyo pia aliwaonya wafanyabiashara wakubwa wanaouza sukari kwa bei ya jumla, akibainisha kuwa wao ndiyo mzizi wa ulanguzi katika bei ya bidhaa hiyo mitaani.

"Nilichogundua katika operesheni hii nyie mnaouza sukari kwa bei ya jumla kwa mfuko mmoja Sh. 140,000 badala ya 128,000, ndiyo chanzo cha tatizo mitaani, kwa sababu kama unamuuzia mtu kwa bei hiyo, yeye atauzaje kwa bei ya rejareja?" alihoji.

Juzi, Bodi ya Sukari Tanzania (SBT), ilikamata shehena ya sukari ikiwa imefichwa kwenye baadhi ya maghala ya wafanyabiashara wakubwa katika Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, zaidi ya tani 23.

Kiasi hicho cha sukari kilikuwa ni kinahusisha sukari inayotokana na viwanda vya ndani na ile iliyoagizwa nje ya nchi ikiuzwa kwa bei ya ulanguzi, tofauti na bei elekezi iliyotangazwa na serikali wiki iliyopita.

Katika operesheni hiyo, Ofisa Mwandamizi wa Udhibiti wa SBT, Faustine Mgimba, alisema wamebaini sukari hiyo ilikuwa ikiuza kwa walaji kwa bei ya rejareja ya Sh. 3,400 tofauti na bei elekezi ya Sh. 2,700 kwa kilogramu moja kwa mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Pwani, Tanga na Morogoro.

Bei ya sukari kwa kila mkoa kwenye mabano ukianza na Dar es Salaam ni (Sh. 2,600), Iringa, Njombe, Mwanza, Simiyu, Shinyanga, Geita, Singida, Tabora na Dodoma (Sh. 2,900), Lindi na Mtwara (Sh. 2,800), Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Pwani, Tanga na Morogoro (Sh. 2,700), Songwe, Mbeya, Mara, Kagera (Sh. 3,000), Rukwa, Katavi, Ruvuma na Kigoma (Sh. 3,200).

# Wagonjwa corona Zanzibar sasa 105

**Na Romana Mallya**

IDADI ya wanaougua ugonjwa wa virusi vya corona Tanzania imefikia 306, baada ya wagonjwa wapya saba kuongezeka jana visiwani Zanzibar.

Kwa mujibu wa taarifa ya Waziri wa Afya visiwani humo, Hamad Rashid Mohammed, wagonjwa wapya walioongezeka ni saba na kufanya kwa sasa Zanzibar kuwa na wagonjwa 105 kutoka 98 waliotolewa taarifa Aprili 24.

Waziri Mohammed alisema wagonjwa hao wapya wote ni Watanzania na wametokea Unguja.

"Jumla ya watu 36 wameruhusiwa kwenda nyumbani baada ya dalili zao za maradhi kuondoka ikiwamo homa, kikohozi, kifua kubana na kuumwa na kichwa," alisema.

Waziri huyo alisema watu hao wameshauriwa waendelee kubaki nyumbani kwa muda wa siku 14 huku wataalamu wa afya wakiendelea kuwafuatilia kabla ya kuruhusiwa kurudi kwenye shughuli zao za kawaida.

"Tunaendelea kuwashauri wananchi waendelee kuchukua tahadhari zote za kujikinga na ugonjwa huu wa corona ikiwa ni pamoja na unawaji wa mikono kwa maji tiririka na sabuni, kuepuka mikusanyiko hasa mwezi huu wa Mtukufu wa Ramadhani," alisema.

Waziri huyo pia aliwataka wananchi wenye dalili za homa kali, kukohoa na kupiga chafya, wajitokeze kwenye vituo cha afya au kupiga simu namba 190.


**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**President's Office – State House**
**TANZANIA SOCIAL ACTION FUND**

**EXTENSION OF DEADLINE FOR SUBMISSION OF TENDERS**

The Tanzania Social Action Fund would like to inform prospective bidders and the general public that the deadline date for submission of the under listed tenders and public opening is further extended from 4th May, 2020 to 5th June, 2020

i. Tender No.TZ-TASAF-148779-GO-RFB to Supply ICT Consumables
ii. Tender No.TZ-TASAF-148787-GO-RFB to Supply Stationery
iii. Tender No. TZ-TASAF-148782-GO-RFB to Supply Motor Vehicle Spare Parts
iv. Tender No. TZ-TASAF-161184-NC-RFB for Printing Handbooks, Manuals, Publicity Materials and Reports

The Executive Director,
Tanzania Social Action Fund,
4th Floor, PSSSF Plaza, JakayaMrishoKikwete Road,
P. O. Box 2719,
Dodoma, Tanzania


# Jaji Ramadhani atakavyokumbukwa

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amemlilia Jaji Mkuu mstaafu wa Tanzania, Augustino Ramadhani, aliyefariki jana, na kumwelezea kuwa atakumbukwa kwa uongozi uliotukuka na ulioshadidishwa na umahiri wake.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa, Jaji Mkuu (mstaafu) Ramadhani alifariki jana asubuhi katika hospitali ya Aga Khan, Dar es Salaam. Katika taarifa hiyo, Rais Magufuli alituma salamu za rambirambi kwa Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Hamis Juma na waumini wa Kanisa la Anglikana kutokana na kifo hicho.

Jaji Mkuu mstaafu Ramadhani enzi za uhai wake alishika nyadhifa mbalimbali serikalini na Desemba 28, 2013 alisimikwa kuwa mchungaji wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Zanzibar baada ya kuwa shemasi kwa muda wa miezi sita na hadi anafariki alikuwa mchungaji.

Katika taarifa hiyo, Rais Magufuli amempa pole Jaji Mkuu Juma na amemwomba kufikisha salamu zake za pole kwa familia ya marehemu, mahakimu na wafanyakazi wote wa mahakama pamoja na waumini wa Kanisa la Anglikana kwa kuondokewa na mpendwa wao.

**WASIFU WAKE**

Machi 1970, baada ya kumaliza Chuo Kikuu, Augustino alijiunga na Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ).

Mwanzoni mwa mwaka 1978, Rais wa pili wa Zanzibar, Alhaj Abdou Jumbe Mwinyi, alimteua kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, kikiwa moja ya vyeo vya juu kisiwani humo na mwaka huo huo alipata Shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) katika Sheria za Kimataifa.

Machi 1979, alirudishwa JWTZ na katika vita ya Kagera alipelekwa vitani na jukumu lake kubwa lilikuwa kuendesha mahakama za kijeshi.

Januari 1980, aliapishwa kuwa Jaji Mkuu wa Zanzibar akiwa Luteni Kanali na alihudumu cheo hicho hadi mwaka 1989 na kuteuliwa na Rais wa awamu ya pili wa Ali Hassan Mwinyi kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania.

Mwaka 1993, Rais Mwinyi alimteua kuwa Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na aliitumikia nafasi hiyo hadi mwaka 2003.

Ilipofika mwaka 1997, alistaafu rasmi JWTZ akiwa na cheo cha Brigedia Jenerali na mwaka 2001 aliteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki na kuhudumu hadi mwaka 2007.

Mwaka 2002 hadi 2007, aliteuliwa kuwa Makamu wa Mwenyekiti Tume ya Uchaguzi, Zanzibar (ZEC) na alisomea uchungaji Chuo Kikuu cha London nchini Uingereza ambapo mwaka 2004 alipata Shahada ya Uchungaji.

Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, alimteua kuwa Jaji Mkuu wa Tanzania mwaka 2007 na kuhudumu hadi mwaka 2010 baada ya kufikisha miaka 65 na aliteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu.

Juni 15 2015, alichukua fomu ya kugombea uraisi kupitia chama cha mapinduzi na kuwa mmoja wa wagombea 42 na Julai 11. Hadi anafariki dunia, alikuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Iringa (UoI).



## DK. REGINALD ABRAHAM MENGI

"Uwoga ni mojawapo ya adui wa mafanikio"

# Tamwa yamuenzi kwa usawa wa haki za binadamu nchini

**Na Gwamaka Alipipi**

MKURUGENZI Mtendaji wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa), Dk. Rose Reuben, anamzungumzia Dk. Reginald Mengi kwa jitihada zake za kupigania haki za wanawake na watoto kupitia vyombo vyake vya habari kwa kushirikiana na chama hicho.

"Magazeti yake, televisheni pamoja na redio zake vilifanya kazi kubwa kupigania haki za wanawake na watoto, tuliweza kufanya kazi na vyombo hivyo kwa kurusha taarifa zinazotetea haki za wanawake na watoto pamoja na matangazo ya kuhamasisha kutokomeza ukatili dhidi yao," anasema Dk. Rose.

Anasema alikuwa mstari wa mbele kuhakikisha waandishi wa habari na tasnia nzima inapata ajira kwa wingi kupitia vyombo vyake vya habari.

Mchango wake mkubwa katika sekta ya habari ulikuza vyombo vya habari nchini na kujipatia sifa nyingi. Katika jitihada zake hizo, Rose anasema Dk. Mengi alikuwa anapenda kuona tasnia ya habari inasonga mbele kila siku, hakupenda kuiona inarudi nyuma.

"Sisi Tamwa tunamkumbuka Dk. Mengi kwa mchango wake mkubwa alioutoa katika sekta ya habari kwa kukuza vyombo vya habari. Waandishi wa habari na tasnia nzima ilipata ajira kwa wingi kupitia vyombo vyake vya habari."

"Nakumbuka tangazo la 'Sidanganyiki' lililokuwa linarushwa na kituo cha ITV ambalo lilikuwa linawaasa watoto wa kike wasidanganyike na mafataki kwa kupata ujauzito. Ni tangazo ambalo lilisaidia sana kupunguza mimba za utotoni, lakini pia matangazo ya kupunguza mimba za utotoni nayo tuliyatangaza sana katika vyombo vyake vya habari."

Kupitia vyombo hivyo, Rose anasema habari nyingi za ukatili wa kijinsia zilipewa nafasi kubwa kwa kuripotiwa na kuelimisha jamii kwa sababu alipenda kupigania haki ya wanawake na watoto.

Anasema ameacha alama ya haki za binadamu na usawa wa jinsia kwa Watanzania ikiwa imeeleweka kwa kiasi kikubwa.

"Kwa sababu awali suala hilo lilikuwa halizungumzwi sana, lakini kupitia vyombo vyake vya habari vilisaidia sana angalau suala la jinsia linaeleweka kwa wanawake na wanaume."

Kurushwa kwa taarifa kwenye vyombo hivyo, Rose anasema kumesaidia Watanzania sasa kufahamu kuwa usawa wa kijinsia ni usawa wa kijamii na siyo usawa wa kibailojia ambao watu wamekuwa wakishindana kimabavu.

Amewakumbusha wamiliki wengine wa vyombo vya habari kuendelea kuwathamini waandishi wa habari, kama ilivyokuwa kwa Dk. Mengi.



Dk Reginald Mengi akilakiwa na wanachama wa kikundi cha walimu cha kuweka na kukopa jijini Dar es Salaam. **PICHA ZOTE NA MPIGAPICA WETU**

> Kwa sababu awali suala hilo lilikuwa halizungumzwi sana, lakini kupitia vyombo vyake vya habari vilisaidia sana angalau suala la jinsia linaeleweka kwa wanawake na wanaume.



Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa), Dk. Rose Reuben.

"Uandishi wa habari ni kazi, ni taaluma na siyo taaluma ambayo kila mtu anaweza kuifanya. Wamiliki wa vyombo vya habari waendelee kuwathamini waandishi wa habari wanawake na wanaume, waendele kuthamini kazi wanazozifanya, na waithamini habari."

"Kama Tamwa tunasisitiza wamiliki wa vyombo vya habari waendelee kuthamini, kutoa taarifa za kijinsia, kuzuia ukatili wa wanawake na watoto, wapaze sauti za wanawake ili tufikie maendeleo endelevu." Anasisitiza Rose.

Anasema Tamwa inamuenzi Dk. Mengi kwa kuwatetea watu wasiojiweza wakiwamo watoto na wanawake wenye ulemavu.

Tamwa pia inawajengea uwezo wanawake wanahabari kitaaluma kwa kuwawezesha mikopo isiyo na riba ili wajiendeleza kielimu na kuendelea kutetea wanyonge ambao sauti zao hazisikiki.

Dk. Rose anasema Dk. Mengi alikuwa mfano wa kuigwa kwa kufanya mambo makubwa kwenye tasnia ya habari kwa sababu hakuwa mbaguzi katika kuwapatia uwezo waandishi wa habari hata wale ambao hawakuwa katika vyombo vyake.

"Dk. Mengi alikuwa amewajengea uwezo waandishi wote bila ya kuwabagua pamoja na kuwaendeleza kimasomo," anasisitiza Dk. Rose.

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

**Amana Bank**
*Pamoja, katika njia sahihi*

**WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI 2020**

| | SHS '000<br>Robo Mwaka<br>31- 03 - 2020 | SHS '000<br>Robo Mwaka<br>31 - 12 - 2019 |
|---|---|---|
| **A. MALI** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 9,749,917 | 12,308,710 |
| 2. Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 38,177,875 | 18,756,238 |
| 3. Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 0 | 0 |
| 4. Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 3,723,275 | 5,854,327 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 232,439 | 65,494 |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 1,209,732 | 19,223,998 |
| 10. Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 151,523,284 | 162,644,151 |
| 12. Mali Nyingine | 9,408,487 | 9,551,392 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| 14. Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 9,165,754 | 9,677,365 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **223,190,763** | **238,081,675** |
| | 0 | 0 |
| **B. DHIMA** | 0 | 0 |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,620,850 | 7,246,575 |
| 18. Amana za Wateja | 174,250,080 | 183,137,292 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20. Amana Maalumu | 11,876,958 | 13,170,304 |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 116,739 | 110,250 |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 184,846 | 772,342 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 51,179 | 97,441 |
| 27. Dhima Nyingine | 7,715,949 | 6,422,850 |
| 28. Madeni | 0 | 0 |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | 195,816,601 | 210,957,053 |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **27,374,162** | **27,124,622** |
| | | |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | | |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 39,697,089 | 39,697,089 |
| 32. Akiba ya Mtaji | 8,409,752 | 10,624,547 |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (20,982,218) | (23,928,976) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 249,539 | 731,962 |
| 35. Akaunti Nyingine za Mtaji | 0 | 0 |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **27,374,162** | **27,124,622** |
| | | |
| 38.Dhima Zisizo Dhahiri | 10,754,523 | 13,950,647 |
| 39. Mikopo Chechefu | 14,984,006 | 18,910,750 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 2,448,763 | 2,167,030 |
| 41. Mali Nyingine Chechefu | | |
| | | |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 12% | 11% |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 9.7% | 9.2% |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 82% | 80% |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 69% | 67% |
| (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 70% | 76% |
| (vi) Ongezeko la Amana | -8% | 2% |
| (vii) Ongezeko la Mali | -6.3% | 3% |

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2020**

| | SHS'000<br>Robo ya Mwaka sasa | SHS'000<br>Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | SHS'000<br>Limbikizo la Mwaka wa sasa | SHS'000<br>Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|
| | 31 - 03 - 2020 | 31 - 03 - 2019 | 31 - 03 - 2020 | 31 - 03 - 2019 |
| 1. Faida itokanayo na Mikopo | 4,842,620 | 4,963,159 | 4,842,620 | 4,963,159 |
| 2. Gawio la Faida kwa waweka Amana | (1,409,066) | (1,526,253) | (1,409,066) | (1,526,253) |
| 3. Mapato Halisi ya Faida (1kutoa 2) | 3,433,554 | 3,436,906 | 3,433,554 | 3,436,906 |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | -274,776 | 162,265 | -274,776 | 162,265 |
| | | | | |
| **6. Faida isiyotokana na Mikopo:** | **1,476,688** | **1,827,435** | **1,476,688** | **1,827,435** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 271,753 | 581,929 | 271,753 | 581,929 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 1,204,935 | 1,245,506 | 1,204,935 | 1,245,506 |
| 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 6.4 Mapato Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **7. Gharama za uendeshaji:** | **(4,812,571)** | **(4,564,967)** | **(4,812,571)** | **(4,564,967)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (2,147,358) | (2,169,599) | (2,147,358) | (2,169,599) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7.3 Gharama Nyingine | (2,665,213) | (2,395,368) | (2,665,213) | (2,395,368) |
| 8. Faida /(Hasara) ya Uendeshaji | 372,447 | 537,109 | 372,447 | 537,109 |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | (122,908) | (177,246) | (122,908) | -177,246 |
| **10. Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **249,539** | **359,863** | **249,539** | **359,863** |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **249,539** | **359,863** | **249,539** | **359,863** |
| | | | | |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 235 | 218 | 235 | 218 |
| 14. Mapato kwa Hisa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 15. Idadi ya Matawi | 9 | 9 | 9 | 9 |
| | | | | |
| BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.11% | 0.26% | 0.11% | 0.26% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1% | 2% | 1% | 2% |
| (iii) Uwiano wa Gharama za uendeshaji na Mapato Ghafi | 76% | 67% | 76% | 67% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya yatokanayo na Mikopo na Wastani wa Mali | 2% | 3% | 2% | 3% |
| | | | | |

**TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 MACHI 2020**

| | SHS'000<br>Robo Mwaka<br>Mwaka wa sasa<br>31 - 03 - 2020 | SHS'000<br>Robo Mwaka<br>Uliopita<br>31 - 12 - 2019 |
|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 372,447 | 928,042 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | 0 | 0 |
| - Hasara Katika Mali | 288,269 | 2,664,455 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 0 | 0 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 12,078,165 | (10,449,554) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (15,806,282) | 7,248,471 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| - Mabadiliko ya kiwango kinachohitajika na banki kuu kisheria | 317,474 | 1,713,306 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 665,830 | (1,216,541) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (151,948) | 118,552 |
| - Kodi Iliyolipwa | (32,822) | (112,828) |
| - Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 |
| Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji | (2,268,867) | 893,903 |
| | | |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | 0 | 0 |
| Gawio Lililopokewa | 0 | 0 |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (322,844) | (1,754,341) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | (73,132) | (1,107,000) |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji | (395,976) | (2,861,341) |
| | | |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | 0 | 0 |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 0 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | 0 | 0 |
| | | |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (2,664,843) | (1,967,438) |
| | | |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 42,300,400 | 44,267,838 |
| | | |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **39,635,557** | **42,300,400** |

**TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2020**

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyo-bakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengi-neyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka wa sasa 2019 | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 39,697,089 | 0 | (23,197,014) | 10,624,547 | - | 0 | 27,124,622 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 249,539 | 0 | 0 | 0 | 249,539 |
| Share zilizouzwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 2,214,795 | (2,214,795) | 0 | 0 | 0 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Salio la mwisho wa mwaka | 39,697,089 | 0 | (20,732,679) | 8,409,752 | 0 | 0 | 27,374,161 |
| | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mwaka Uliopita 2019 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Salio la mwanzo wa Mwaka | 39,697,089 | 0 | (17,465,000) | 2,843,597 | 1,316,975 | 0 | 26,392,661 |
| Salio la mwanzo la bamadilio ya utaraibu wa kihasibu namba 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 731,962 | 0 | 0 | 0 | 731,962 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (7,780,950) | 7,780,950 | 0 | 0 | 0 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 1,316,975 | 0 | (1,316,975) | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Salio la mwisho wa mwaka | 39,697,089 | 0 | (23,197,014) | 10,624,547 | - | 0 | 27,124,622 |

Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

Jina na cheo

**Dr. Muhsin Salim Masoud**
(Mkurugenzi mtendaji) — Imesainiwa Machi 31, 2020

**CPA Saidi Mbaruku**
(Mkuu wa Fedha) — Imesainiwa Machi 31, 2020

**Mwinyi Sekro**
(Mkuu wa Ukaguzi) — Imesainiwa Machi 31, 2020

Benki ilitozwa faini ya SH 406,000 kwa kutofuata utaratibu wa utayarishaji, ufungaji na uandaaji wa fedha kama ilivyoanishwa kwenye sheria husika ya Benki kuu ya mwaka 2015

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

**Abdallah Nahdi**
(Mwenyekiti) — Imesainiwa Machi 31, 2020

**Salem Balleith**
(Mkurugenzi) — Imesainiwa Machi 31, 2020




You can now withdraw cash at any bank's ATM that has Mastercard system, if you have

Amana Bank
Together, on the right path

mastercard

Customer service number 0657 980 000 | 0657 980 000 | /amanabanktz | /amanabank

# Tariff Guide

**Amana Bank**
*Together, on the right path*

| | PRODUCT/SERVICES | LOCAL CURRENCY (TZS) | FOREIGN CURRENCY(USD, EUR, GBP) |
|---|---|---|---|
| 1 | **SAVINGS ACCOUNT (Personal/Joint/Annisaa** | | |
| | Minimum Opening balance | 20,000 | USD, EUR, GBP 100 |
| | Account Maintenance balance | 10,000 | USD, EUR, GBP 100 |
| | Profit Participation Balance (Min. Daily balance) | 100,000 | USD, EUR, GBP 1,000 |
| | Limit on Withdrawal | No limit | No limit |
| | Monthly Maintenance Fee | 1,500 | USD, EUR, GBP 4 |
| | Over the counter withdrawal fee | 3,500 | Below USD, EUR, GBP 1,000 - 0% Over USD, EUR, GBP 1,000 - 0.25% |
| | Over the counter withdrawal limit (above TZS 10,000,000) | 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | N/A |
| | Over the counter balance enquiry fee | 500 | USD, EUR, GBP 1 |
| | Bank Statements (monthly) | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP 4 Per Statement |
| | Bank Statements above twelve months | 20,000 per statement | USD, EUR, GBP 10 Per Statement |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| 2 | **STUDENT ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 10,000 | N/A |
| | Account Maintenance balance | 10,000 | N/A |
| | Profit Participation Balance (Min. Daily balance) | 100,000 | N/A |
| | Limit on Withdrawal | No limit | N/A |
| | Monthly Maintenance Fee | Free | N/A |
| | Over the counter withdrawal fee | Free | N/A |
| | Over the counter withdrawal limit ( above TZS 10,000,000 ) | Above 10,000,000 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | N/A |
| | Over the counter balance enquiry fee | Free | N/A |
| | Bank Statements (monthly) | Free | N/A |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | N/A |
| | Bank Statements above twelve months | 20,000 per statement | N/A |
| | Electronic Statement | Free | N/A |
| 3 | **KILIMANJARO DIASPORA ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 200,000 | USD, EUR, GBP 100 |
| | Account Maintenance balance | 10,000 | USD, EUR, GBP 100 |
| | Profit Participation Balance (Min. Daily balance) | 100,000 | USD, EUR, GBP 1,000 |
| | Limit on Withdrawal | No limit | No limit |
| | Monthly Maintenance Fee | 1,500 | USD, EUR, GBP 4.0 |
| | Over the counter withdrawal fee | 1,500 | 1.2% minimum USD, EUR, GBP 6 |
| | Over the counter withdrawal limit ( above TZS 10,000,000 ) | Above 10,000,000 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | N/A |
| | Over the counter balance enquiry fee | 500 | USD, EUR, GBP 1 |
| | Bank Statements (monthly, quarterly, annually) | Free | USD, EUR, GBP 4.0 Per Statement |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP 10 Per Statement |
| | Bank Statements above twelve months | 20,000 per statement | Free |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| 4 | **ASHRAF ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 1,000,000 | USD, EUR, GBP Equivalent |
| | Account Maintenance balance | 2,000,000 | USD, EUR, GBP/GBP/EURO 1,000 |
| | Profit Participation Balance (Min. Daily balance) | 100,000 | USD, EUR, GBP 1,000 |
| | Monthly Maintenance Fee | 14,000 | USD, EUR, GBP/GBP/EURO 10 |
| | Over the counter withdrawal fee | 3,500(Savings Account), 1,500(Current Account) | Below USD, EUR, GBP 1,000 - 0% Over USD, EUR, GBP 1,000 - 0.25% |
| | Over the counter withdrawal limit (above TZS 10,000,000) | 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | N/A |
| | Bank Statements (monthly) | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP 4.0 Per Statement |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| | Hajj Time SMS Alert | Free | Free |
| 5 | **BODABODA ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 10,000 | N/A |
| | Account Maintenance balance | 10,000 | N/A |
| | Profit Participation Balance (Min. Daily balance) | 100,000 | N/A |
| | Limit on Withdrawal | No limit | N/A |
| | Monthly Maintenance Fee | Free | N/A |
| | Over the counter withdrawal fee | 1,500 | N/A |
| | Over the counter withdrawal limit ( above TZS 10,000,000 ) | Above 10,000,000 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | N/A |
| | Over the counter balance enquiry fee | 500 | N/A |
| | Bank Statements (monthly) | Free | N/A |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | N/A |
| | Bank Statements above twelve months | 20,000 per statement | N/A |
| | Electronic Statement | Free | N/A |
| 6 | **NAFUU ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 10,000 | N/A |
| | Account Maintenance balance | 10,000 | N/A |
| | Monthly Maintenance Fee | Free | N/A |
| | Over the counter withdrawal fee | From 0 to 50,000 - TZS 1,500 From 50,001 to 100,000 - TZS 2,000 From 100,001 to 200,000 - TZS 2,500 From 200,001 to 300,000 - TZS 3,000 From 300,001 to Above - TZS 3,500 | N/A |
| | Over the counter withdrawal limit ( above TZS 10,000,000 ) | Above 10,000,000 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | N/A |
| | Over the counter balance enquiry fee | Free | N/A |
| | Bank Statements (monthly) | Free | N/A |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | N/A |
| | Bank Statements above twelve months | 20,000 per statement | N/A |
| | Electronic Statement | Free | N/A |
| 7 | **HAJJ & UMRAH SAVINGS ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 10,000 | USD, EUR, GBP 50 |
| | Account Maintenance balance | 10,000 | USD, EUR, GBP 50 |
| | Profit Participation Balance (Min. Daily balance) | 100,000 | USD, EUR, GBP 1,000 |
| | Limit on Withdrawal | Twice Annually | Twice Annually |
| | Monthly Maintenance Fee | Free | Free |
| | Over the counter withdrawal fee | Free | Free |
| | Bank Statements (monthly) | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP 4 Per Statement |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| | Hajj Time SMS Alert | Free | Free |
| 8 | **NURU SAVINGS ACCOUNT (Children Account)** | | |
| | Minimum Opening balance | 10,000 | USD, EUR, GBP 50 |
| | Account Maintenance balance | 10,000 | USD, EUR, GBP 50 |
| | Profit Participation Balance (Min. Daily balance) | 100,000 | USD, EUR, GBP 1,000 |
| | Limit on Withdrawal | Four times in a year | Four times in a year |
| | Charge on withdrawal exceeding 4 times a year | 12,000 | USD, EUR, GBP 6 |
| | Monthly Maintenance Fee | Free | Free |
| | Over the counter withdrawal limit (above TZS 10,000,000) | 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | N/A |
| | Bank Statements (monthly) | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP 4 Per Statement |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| 9 | **SALARY SAVINGS ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 0 | 0 |
| | Account Maintenance balance | 2,000 | USD, EUR, GBP 5 |
| | Profit Participation Balance (Min. Daily balance) | 100,000 | USD, EUR, GBP 1,000 |
| | Monthly Maintenance Fee | 1,500 | USD, EUR, GBP 1.5 |
| | Over the counter withdrawal limit (above TZS 10,000,000) | 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | NA |
| | Over the Counter limit withdrawal Fee | 2,500 | Below USD, EUR, GBP 1,000 - 0% Over USD, EUR, GBP 1,000 - 0.25% |
| | Bank Statements (monthly) | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP 4 Per Statement |
| | Electronic Statement | Free | NA |
| 10 | **PERSONAL CURRENT ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 100,000 | USD, EUR, GBP 100 |
| | Account Maintenance balance | 50,000 | USD, EUR, GBP 50 |
| | Monthly Maintenance Fee | 11,000 | USD, EUR, GBP 11 |
| | Over the counter withdrawal fee | 1,500 | Below USD, EUR, GBP 1,000 - 0% Over USD, EUR, GBP 1,000 - 0.25% |
| | Bank Statements (monthly) | Free | Free |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP 4 Per Statement |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| 11 | **CORPORATE CURRENT ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 100,000 | USD, EUR, GBP 500 |
| | Account Maintenance balance | 50,000 | USD, EUR, GBP 200 |
| | Monthly Maintenance Fee | 15,000 | USD, EUR, GBP 15 |
| | Over the counter withdrawal fee | 2500 | Below USD, EUR, GBP 1,000 - 0.5% Over USD, EUR, GBP 1,000 - 0.5% |
| | Activation of Dormant Account | Free | Free |
| | Certificate of Balance to Auditors/Reference letters | 10,000 | USD, EUR, GBP 5 |
| | Bank Statements (monthly) | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP 4 Per Statement |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| 12 | **BIASHARA CURRENT ACCOUNT (SMEs)** | | |
| | Minimum Opening balance | 100,000 | USD, EUR, GBP 100 |
| | Account Maintenance balance | 50,000 | USD, EUR, GBP 50 |
| | Monthly Maintenance Fee | 13,000 | USD, EUR, GBP 13 |
| | Over the counter withdrawal fee | 1,500 | Below USD, EUR, GBP 1,000 - 0.5% Over USD, EUR, GBP 1,000 - 0.5% |
| | Certificate of Balance to Auditors/Reference Letters | 10,000 | USD, EUR, GBP 5 |
| | Activation of Dormant Account | Free | Free |
| | Bank Statements (monthly) | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP 4 Per Statement |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| 13 | **NGO CURRENT ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 100,000 | USD, EUR, GBP 100 |
| | Account Maintenance balance | 0 | 0 |
| | Monthly Maintenance Fee | 0 | 0 |
| | Over the counter withdrawal fee | 1,500 | Below USD, EUR, GBP 1,000 - 0% Over USD, EUR, GBP 1,000 - 0.25% |
| | Certificate of Balance to Auditors/Reference Letters | 10,000 | USD, EUR, GBP 5 |
| | Activation of Dormant Account | Free | Free |
| | Bank Statements (monthly) | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 2,000 Per Page | USD, EUR, GBP 1 Per Page |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| 14 | **IHSAAN CURRENT ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 0 | 0 |
| | Account Maintenance balance | 0 | 0 |
| | Over the counter withdrawal fee | 0 | 0 |
| | Bank Statements (monthly) | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 2,000 Per Page | USD, EUR, GBP 1 Per Page |
| | Monthly Maintenance Fee | Free | Free |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| 15 | **FIXED/TERM DEPOSITS** | | |
| | Minimum Opening balance | 1,000,000 | USD, EUR, GBP 1,000 |
| | Profit Participation Balance | Amount placed | Amount placed |
| | Limit on Withdrawal | Until maturity | Until maturity |
| | Certificate of Investment | Free | Free |
| | Certificate of Balance to Auditors | 50,000 | USD, EUR, GBP 25 |
| 16 | **OTHER DEPOSIT SERVICES** | | |
| | Over the counter balance enquiry fee (for all a/cs) | 500 | USD, EUR, GBP 1 |
| | Account Closure Fee (for all account types) | Free | Free |
| | Activation of Dormant Accounts | Free | Free |
| | Cash deposits for all account types | Free | Free |
| | Cash deposits for small denominations (less than USD, EUR, GBP 50) | N/A | 5% of total |
| | Withdraw by using counter cheque :Forgotten/ loss/stale | 15,000 | USD, EUR, GBP 7 |
| 17 | **CHEQUE BOOKS** | | |
| | Issuance: 100 leaves cheque book | 60,000 | USD 35 |
| | Issuance: 50 leaves cheque book | 30,000 | USD 20 |
| | Issuance: 25 leaves cheque book | 15,000 | USD 10 |
| | Stop Payment of Cheque | 40,000 | USD 35 |
| | Unpaid Cheque - Insufficient fund and uncleared effect | 100,000 | USD 50 |
| | Unpaid Cheque - technical reason | Free | Free |
| | Uncollected Cheque book after advice period of 3 months | 20,000 | USD 12 |
| 18 | **BANKERS CHEQUE/ PAYMENT ORDER/ BANK / DEMAND DRAFTS** | | |
| | Issuance: For Account holder | 30,000 | USD 25 |
| | Cancellation: For Account holder | 30,000 | USD 25 |
| | Stop Payment | 40,000 | USD 35 |
| 19 | **ATM/DEBIT CARD** | | |
| | Issuance of ATM card fee | 10,000 | N/A |
| | Issuance Nafuu ATM card | Free | N/A |
| | Replacement of lost/stolen or damaged card | 10,000 | N/A |
| | Replacement of PIN | N/A | N/A |
| | Annual fee | 30,000 | N/A |
| | ATM card activation | Free | N/A |
| | Blocking/Hotting ATM card | Free | Free |
| | ATM Cash Withdrawal fee per transaction at AMANA BANK and CRDB | From 0 to 50,000 - 1,500 From 50,001 to 100,000 - 1,800 From 100,001 to 200,000 - 2,100 From 200,001 to 300,000 - 2,500 From 300,001 to 400,000 - 2,800 | N/A |
| | ATM Cash Withdrawal fee per transaction Mastercard local | 4,000 | N/A |
| | ATM Cash Withdrawal fee per transaction Mastercard international | 7,300 | N/A |
| | Nafuu ATM Cash Withdrawal fee | From 0 to 50,000 - 1,500 From 50,001 to 100,000 - 1,800 From 100,001 to 200,000 - 2,100 From 200,001 to 300,000 - 2,500 From 300,001 to 400,000 - 2,800 | N/A |
| 20 | **FUND TRANSFERS/REMITTANCES** | | |
| | Internal Transfers within Amana Bank | Free | Free |
| | Cross border transfers (TT, SWIFT) - outward USD, EUR, GBP | N/A | USD 50 (If charges are shared), USD 70 (If all charges are born by sender) |
| | Inward Transfers (TT, SWIFT) | Free | USD 12 |
| | Amendment of TISS, SWIFT Message | 12,000 | USD 12 |
| | Amendment of TT, SWIFT Message | N/A | USD 20 |
| | Confirmation | Free | Free |
| | TISS | 12,000 | USD 12 |
| | EFT (Bulk Payments): Out&Inward/salary processing fee | 3,000 per transaction | USD 2 per transaction |
| | Stop Payments (TISS/EFT/SWIFT) | 20,000 | USD 20 |
| 21 | **GUARANTEE & LETTER OF CREDIT CHARGES** | | |
| | Commission on Guarantee/Letter of Credit | Once of 1% facility fee and 0.75% commission per quarter or any part there of | |
| | Commission on Documentary Collection | USD 120 | |
| | Handling documents | USD 100 | |
| | Amendment of LC/Guarante | USD 100 | |
| | Re-issue of guarantee (Loss of Guarantee) | USD 100 | |
| | Cancellation of Guarantee/LC | USD 100 | |
| | Advising LC charge | USD 200 | |
| | Confirmation Rate | Min. USD, EUR, GBP 200/- 0.35% per quarter or any part there of | |
| | Negotiation Rate | Min. USD 100/- 0.125% | |
| | Advising | USD 310 | |
| | Courier | International USD 100, Local USD 50 | |
| | LG Charge | 3.50% per year | |
| 22 | **STANDING ORDERS** | | |
| | Standing Order Instructions within Amana Bank | Free | Free |
| | Standing Order Instructions - Outward | 12,000 per instruction | USD, EUR, GBP 12 per instruction |
| | Standing orders - Cancellation/Stopping | Free | Free |
| | Standing Orders - Amendments | Free | Free |
| | Unpaid Standing Orders | 12,000 per instruction | USD, EUR, GBP 12 per instruction |
| 23 | **INTERNET BANKING** | | |
| | Registration | Free | Free |
| | Equipment (one off) per user | 100,000 | USD 60 |
| | Monthly Service Fee (Corporate) | 15,000 | USD 8 |
| | Monthly Service Fee (Personal) | 6,000 | USD 3.6 |
| 24 | **SMS BANKING** | | |
| | Account Balance Enquiry | 300 | N/A |
| | Ministatement | 300 | N/A |
| | Cheque Status Enquiry | 300 | N/A |
| | Cheque book request | 300 | N/A |
| | Internal fund transfer | 1,500 | N/A |
| | Account activity Alert | 200 | N/A |
| | Airtime recharge | Free | N/A |
| | Utility bill payment | Free | N/A |
| | All Mobile Network Operators | Up to 100,000 - TZS 1500 100,001 - 500,000 - 2500 500,001 - 1,000,000 - 3,500 1,000,001 - 3,000,000 - 4,500 3,000,001 - 5,000,000 - 5,500 5,000,001 - Above - 7,500 | N/A |
| 25 | **OTHER SERVICES** | | |
| | SMS Alert fee per transaction | 200 | N/A |
| | Search Old Documents/Document Retrieval charges - between one months and six months | 10,000 | USD, EUR, GBP 5 |
| | Search Old Documents/Document Retrieval charges - above six months | 30,000 | USD, EUR, GBP 15 |
| | Retrieval charges on stale Cheques | 20,000 | USD, EUR, GBP 10 |
| | Quarterly dormant charges | N/A | N/A |
| | Electronic Schedule of Charges Fee | Free | Free |
| | Change of Address/Telephone numbers | Free | Free |
| | Status opinion (Reference letter,certificate of balance of Auditors,Embassy letter) | 10,000 | USD, EUR, GBP 5 |
| | Salary processing | 3,000 Per Transaction | USD, EUR, GBP 2 Per Transaction |
| | Bulk payment Service | 1,300 per transaction | N/A |

**Amana Bank**
*Together, on the right path*

***Home of unsecured BID Guarantees***

**Visit our Branches or Call us Now 0657 980 000**

0657 980 000 /amanabanktz /amanabank

*Terms & conditions apply



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunaweza kuishusha zaidi bei ya barakoa

**MLIPUKO** wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu (COVID-19) ambayo inasababishwa na virusi vya corona, imepaisha bei ya barakoa, na kuwapa wakati mgumu watu wa kipato cha chini.

Uvaaji wa barakoa ni sehemu ya tahadhari inayoelekezwa na wataalamu wa afya katika kudhibiti maambukizo ya virusi vya corona. Kama ulivyo utamaduni wa wafanyabiashara nchini kutumia matatizo kujinufaisha, ndivyo walivyofanya katika suala la barakoa. Kutokana na mahitaji makubwa ya barakoa kwa sasa, watengenezaji hususan wa viwandani, sasa wameligeuza janga la corona kama fursa kwao, kutokana na kuziuza kwa bei ya juu kupita kiasi.

Wanafanya hivyo bila kuwajali Watanzania wa kupato cha juu, ambao hawana uwezo wa kuzinunua kwa bei hiyo. Kwa bahati serikali imelibaini tatizo hili na kuanza kuchukua hatua, ikiwamo ya kutangaza bei elekezi ili kila Mtanzania awe na uwezo wa kununua kujikinga dhidi ya maambukizo.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, amesema atachukua hatua kwa Taasisi zisizo za kiserikali (NGO) zinazouza barakoa kwa gharama kubwa.

Bashungwa alitoa tahadhari hiyo mkoani Arusha juzi, alipotembelea viwanda vya kuzalisha nguo vya Sunflug na A to Z kuangalia hali ya uzalishaji wa barakoa katika viwanda hivyo.

Alizionya NGO zilizoomba kibali cha kuzalisha barakoa kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania, lakini badala yake alisema wanauza barakoa kwa Sh. 2,500 hadi 3,000.

Kwa mujibu wa Waziri huyo, wazalishaji hao wamekuwa wakitoa masharti kupitia mitandao ya kijamii kuwa hawauzi barakoa chini ya bei hiyo. Bashungwa alisema asingewataja watu hao kwa wakati huo, lakini akiona wanauza kwa bei kubwa hatasita kuwachukulia hatua, maana wanakwenda kuomba vibali, wakati wanatafuta mtaji.

Waziri Bashungwa alitangaza beo elekezi ya barakoa kuwa zote ziuzwe kwa bei isiyozidi Sh. 1,500 badala ya bei ya sasa iliyokuwa sokoni ya Sh. 2,500, ambayo Watanzania wengi inawapa changamoto ya kumudu. Ingawa alitumia lugha ya kidiplomasia kuwafikishia ujumbe wazalishaji hao wanaotanguliza mbele faida binafsi badala ya maskahi ya Watanzania, bila shaka ujumbe aliowatumia ni kuwa wakiendelea kukaidi kuzingatia bei elekezi watachukuliwa hatua kali, ikiwamo wanyang'anywa leseni.

Tunakubaliana na uamuzi wa kutangaza bei elekezi, lakini kwa upande mwingine tunashauri serikali kuwa haina sababu za kupoteza muda wake kuwabembeleza au kupambana na walanguzi wa barakoa.

Ili kuondokana na changamoto ya bei, ambayo wengi hawawezi kumudu, serikali bainabudi kubuni na kuweka mazingira mazuri, ili wazalishaji wengine wajitose katika uzalishaji wa barakoa.

Wajasiriamali wadogo, wakiwamo washonaji wanaweza kuandaliwa na kuwekewa mazingira bora, hatimaye wakazalisha barakoa, ambazo watazIuza kwa bei ya kawaida.

Wakati huu wa mahitaji ya bidhaa hizo, tumeshaona katika maeneo kadhaa hususani jijini Dar es Salaam baadhi ya wajasiriamali wadogo wakitengeneza barakoa, na kweli wengi wameanza kuzichangamkia kutokana na bei yake kuimudu.

Tunaamini pia Shirika la Viwanda Vidogo nchini (Sido), lina uwezo wa kuzalisha barakoa za kutosha na kwa bei ambayo Watanzania wengi wataimudu.

Tunapaswa kujifunzia katika janga la corona kuwa pale zinapotokea changamoto za dharura, tujaribu kutafuta suluhisho haraka. Kwa mfano kama kuna mahitaji ya ghafla, tucheze katika ile misingi ya mahitaji (demand) na supply (usambazaji) kwenda sambamba. Kwa lugha rahisi, tujitahidi kuzalisha kwa wingi na kwa haraka bidhaa ambazo zinakuwa na mahitaji wakati huo, kwa lengo la kuwanyima nafasi waliozoea kutumia fursa hiyo kujinufaisha kwa kujitengenezea faida kubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Jenifer Julius

## Muungwana Lazima Nilonge

# Corona na nzige athari za tabianchi?

**TAATHIRA** ya mabadiliko ya tabianchi ni janga linaloweza kuwa na sura mbalimbali kama vimbunga , mafuriko, ukame na ongezeko la maradhi yakiwamo COVID 19 yanayoitesa dunia kwa sasa.

Licha ya corona kuyapasua vichwa mataifa mbalimbali hasa ukizingatia athari zake ni vifo vingi kwa wakati mmoja na kuumiza uchumi , ni ukweli kuwa kuna haja sasa kuanza kutafakari ongezeko la maradhi kwa wanadamu na mazao ya kilimo kama jambo lenye uhusiano na mabadiliko ya tabianchi.

Ripoti ya tathmini ya mabadiliko ya tabia nchi iliyotolewa na Jopo la kiserikali la kimataifa, linalofanya kazi ya kutathmini mabadiliko ya hali ya hewa kidunia (IPCC) mwaka jana, inasema kama jitihada hazitachukuliwa kufikia mwaka 2030 joto duniani litaongezeka nyuzi 1.5.

Na hali ikiendelea bila kuchukua hatua kufikia mwaka 2052 nyuzi joto zitafikia 2 hali ambayo ni hatari kwa viumbe wote kuanzia ardhini na baharini.

Joto hilo licha ya kuyeyusha theluji, kuongeza kina cha bahari na kutishia hatima ya viumbe habari bila shaka ni chanzo cha kuongeza vimelea vya maradhi kama virusi, viuatilifu na hata kuongeza usugu kwa vimelea na viuatilifu hivyo vinapotibiwa.

Maradhi kama corona ambayo ni virusi vinavyosambaa kwa kasi na kuua haraka iwe kama kengele ya kuiamsha dunia alfajiri na kuanza kujipanga upya kwenye kupunguza shughuli zinazochagiza mabadiliko ya tabianchi.

Jitihada za kusaka tiba na chanjo ya corona zimeikumbusha dunia kuwa ni lazima kukaa pamoja katika kujizatiti kukabiliana na majanga ambayo yanaangamiza ubinadamu kama maradhi hayo na pia ongezeko la joto duniani.

Mojawapo ya hoja iliyojadiliwa na bado inahitaji ufumbuzi wa kina ni Makubaliano ya Paris, hoja yenye mantiki katika muktadha huu, ni kuwekeza katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia na kuiwezesha Afrika na mataifa maskini kushiriki kikamilifu kwenye miradi inayopunguza athari hizo.

Ni jukumu la wanasiasa kuonyesha ukomavu, nia na utayari wa kushiriki kwenye kufanikisha mkataba wa Paris kwani, kuacha mambo kama yalivyo bila kujali mazingira kuna athari kubwa kama ilivyo kwa corona.

Wanasiasa au wakuu wa nchi wanabakia kuwa watendeji pekee kwenye mataifa yao wakihusika na kutoa maelekezo, kuridhia, kutenga fedha na kutekeleza miradi ya kuhifadhi na kutunza mazingira ili kukabiliana na balaa la mabadiliko ya tabianchi.

Dunia ikikaa kimya ikipuuza athari hizo itakuwa inajidanganya kwa sababu leo inashuhudia changamoto nyingi zinazotokana na ongezeko la joto duniani.

Licha ya mvua kunyesha na kusababisha mafuriko , kilimo kinatishiwa na wadudu waharibifu wa mazao na visumbufu visivyosikia viuatilifu likiwa ni tishio kubwa kwa uzalishaji chakula duniani.

Wakati kuna hatari ya kuwapo virusi hatari kama corona Afrika Mashariki ipo kwenye hati hati ya kuwa ukanda wa njaa kutokana na uwepo wa nzige wanaoshambulia mazao mashambani.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) Qu Dongyu, anasema uwepo wa nzige hao ambao wanasambaa kutoka Pembe ya Afrika ni habari mbaya kwenye ukanda huu unaohusisha mataifa ya Afrika Mashariki Sudani, Ethiopia na nchi jirani zilizokusini ya jangwa la Sahara.

Anaeleza fika kuwa sababu kubwa ni mabadiliko ya tabianchi ambayo yameruhusu kuwapo kwa vimbunga vingi vya bahari (nane kuanzia 2019) , mvua nyingi na mafuriko kwenye ukanda, yote hayo yakifanikisha uzalishaji wa kutosha wa wadudu hao na kuweka mazingira bora ya kuzaliana na kusambaa.

Ndiyo maana wakati huu wa corona kutafakari upya njia za kuboresha afya ya dunia na mazingira yake kwa kudhibiti matendo na uwekezaji unaochochea mabadiliko ya tabianchi.

Shime kwa serikali, wadau wa kitaifa na kimataifa ni wakati wa kuanza utekelezaji wa maagizo ya makubaliano ya Paris katika kuwekeza kwenye elimu na miradi mingine ili kufikia mwaka 2030 kuwe na uhakika kuwa pamoja na kupunguza nyuzi joto hazifikii 1.5 ambazo zitaongeza changamoto zaidi.

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

**AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**

*benki kwa maendeleo yako*

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.03.2020
### (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka Mwaka wa sasa 31-Mar-20 | Robo Mwaka Mwaka uliopita 31-Dec-19 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 9,631 | 10,317 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 11,436 | 15,679 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 26,870 | 25,039 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 203 | 211 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 40 | 22 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 7 | (4) |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 81,567 | 84,745 |
| 12 | Mali Nyingine | 11,347 | 10,997 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 20 | 20 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 22,115 | 22,376 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **163,236** | **169,401** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,420 | 3,361 |
| 18 | Amana za Wateja | 110,406 | 107,111 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 0 | 0 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 1 | 2 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 2,766 | 2,820 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 617 | 7,307 |
| 27 | Dhima Nyingine | 22,134 | 15,322 |
| 28 | Madeni | 5,137 | 12,086 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **142,483** | **148,010** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **20,752** | **21,391** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 10,984 | 10,984 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 2,790 | 4,688 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (378) | 0 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 7,356 | 5,719 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **20,752** | **21,391** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 463 | 372 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 18,256 | 16,706 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 9,327 | 9,204 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 73 | 1,461 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 12.7% | 12.6% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 19.8% | 17.8% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 81.2% | 83.9% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 56.5% | 55.5% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 66.6% | 64.9% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 1.2% | -7.0% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -3.6% | 9.1% |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
## KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.03.2020
### (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 31-Mar-20 | Robo ya mwaka Linganishi 31-Mar-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mar-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31-Mar-19 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 6,551 | 6,959 | 6,551 | 6,959 |
| 2 | Gharama za Riba | (1,683) | (1,183) | (1,683) | (1,183) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **4,868** | **5,776** | **4,868** | **5,776** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (123) | (141) | (123) | (141) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **1,317** | **1,873** | **1,317** | **1,873** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 73 | 48 | 73 | 48 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 998 | 1,532 | 998 | 1,532 |
| | 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 246 | 292 | 246 | 292 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(6,439)** | **(7,291)** | **(6,439)** | **(7,291)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (3,315) | (3,761) | (3,315) | (3,761) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (3,124) | (3,530) | (3,124) | (3,530) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(378)** | **217** | **(378)** | **217** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(378)** | **217** | **(378)** | **217** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(378)** | **217** | **(378)** | **217** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 425 | 450 | 425 | 450 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (34) | 25 | (34) | 25 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | **18** | **18** | **18** | **18** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.9% | 1% | -0.9% | 1% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -7.2% | 4% | -7.2% | 4% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 104.1% | 95% | 104.1% | 95% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 17.8% | 22% | 17.8% | 22% |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.03.2020

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2020** | **10,984,416** | **2,431,917** | **4,687,639** | **3,286,944** | **-** | **21,390,916** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | (377,607) | 0 | 0 | (377,607) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (1,897,906) | 1,636,901 | 0 | (261,005) |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | - | 0 | - | - |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.03.2020** | **10,984,416** | **2,431,917** | **2,412,126** | **4,923,845** | **-** | **20,752,304** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2019** | **8,607,136** | **2,431,917** | **7,546,745** | **2,537,257** | **779,217** | **21,902,272** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 217,414 | 0 | 0 | 217,414 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | -678,989 | 633,503 | 0 | -45,486 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | -90,011 | 0 | 90,011 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.03.2019** | **8,607,136** | **2,431,917** | **6,995,159** | **3,170,760** | **869,227** | **22,074,199** |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
## KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2019
### (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31-Mar-20 | Robo Mwaka iliyopita 31-Dec-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mar-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31-Mar-19 |
|---|---|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (378) | (1,226) | (378) | 217 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | - Hasara Katika Mali | 764 | 5,604 | 764 | 418 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 3,178 | (3,922) | 3,178 | 372 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 0 | (3) | 0 | (5) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 1,355 | (7,921) | 1,355 | (5,400) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 1,500 | 1,531 | 1,500 | 6,855 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (6,990) | (599) | (6,990) | (895) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (351) | 3,865 | (351) | (697) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (416) | 0 | (416) | 0 |
| | - Mengineyo (bainisha) | (196) | 2,208 | (196) | 58 |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **(1,532)** | **(463)** | **(1,532)** | **924** |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (46) | (427) | (46) | (186) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | (0) | 3 | (0) | 5 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | **(46)** | **(424)** | **(46)** | **(181)** |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 2,377 | 0 | 0 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | (0) | 0 | (0) | 0 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Mengineyo (bainisha) | (695) | (2,450) | (695) | 0 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(695)** | **(73)** | **(695)** | **0** |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (2,273) | (960) | (2,273) | 743 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 18,624 | 19,584 | 18,624 | 19,584 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **16,351** | **18,624** | **16,351** | **20,327** |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.03.2020**

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

Jina na Cheo Saini Tarehe

Juliana Swai
**(Kaimu Mtendaji Mkuu)**

Bertha Simon
**(Mkuu wa Fedha)**

Chemo Mutani
**(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)**

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

Jina Saini Tarehe

1. Ernest Massawe
2. Dr. Josephat Daniel Lotto





Tafadhali tembelea tawi la Akiba lililo karibu nawe au piga huduma kwa wateja; simu namba: 0746 811 510

## HABARI KITAIFA

# Rufani vigogo Chadema kusikilizwa na warufani, mawakili pande husika

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imesema rufani ya vigogo wanane wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) akiwamo Mwenyekiti wa Taifa, Freeman Mbowe, dhidi ya Jamhuri itasikilizwa na warufani na mawakili wa pande zote mbili na haitaruhusu wasikizaji.

Rufani hiyo ilitajwa jana na Jaji Mfawidhi Lameck Mlacha, huku akibainisha kuwa itasikilizwa mbele ya Jaji Ilvin Mgeta wa mahakama hiyo.

"Siku ya kusikiliza rufani hii wataruhusiwa kuingia warufani na mawakili wao tu. Wasikilizaji wengine hawataruhusiwa kutokana na kuepusha mkusanyika wa kujilinda na maambukizo ya corona," alisema Jaji Mlacha.

Awali upande wa walalamikiwa ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon na Salim Msemo, ulidai kuwa rufani hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na kupanga tarehe ya kusikiliza. Upande wa walalamikaji uliongozwa na Wakili Peter Kibatala.

Mbowe na wenzake wamekata rufani Mahakama Kuu kupinga hukumu ya kulipa faini ya jumla ya Sh. milioni 320 au kwenda jela miezi mitano kwa kila kosa.

Rufani hiyo iliyosajiliwa kwa namba 76 mwaka huu imewasilishwa na wakili wa walalamikaji, Peter Kibatala ikiwa na sababu 14.

Kwa mujibu wa hati ya rufani, walalamikaji wanadai kuwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam ilighafilika kisheria kuwatia hatiani Mbowe na wenzake kwa sababu haikuchambua ushahidi wa Jamhuri wakati wa kuandika hukumu hiyo.

Hoja nyingine, Mahakama ya Kisutu katika hukumu yake haikuonyesha sababu zilizofanya washitakiwa kutiwa hatiani.

"Upande wa Jamhuri ni jukumu lao kuthibitisha makosa bila kuacha shaka na kwamba si kazi ya mshitakiwa kujitetea" ilieleza sehemu ya hoja za walalamikaji.

Hoja nyingine inadai kuwa Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba hakutilia manani utetezi wa washitakiwa akiwamo Esther Matiko na John Mnyika katika ushahidi wa Jamhuri hakuna ulipoeleza kama washitakiwa walikuwapo kwenye tukio.

Pia mahakama inadaiwa ilighafilika kisheria kuwatia hatiani washitakiwa katika shitaka lililokuwa na mashitaka manne ndani yake ikiwamo kufanya maandamano, kusababisha kifo cha Akwilina na kusababisha Askari polisi wawili kujeruhiwa.

Hoja nyingine kwamba mahakama ilipokea CD iliyoonyesha maandamano ya washitakiwa kinyume cha sheria na kwamba utaratibu wa kisheria haukufuatwa kielelezo hicho kilipokelewa kiholela.

Mbali na Mbowe, Matiko, Mnyika washitakiwa wengine ni, Mchungaji Peter Msigwa, Halima Mdee, John Heche, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu, na Mbunge wa Bunda , Esther Bulaya.

Katika kesi ha msingi, Mbowe na viongozi wenzake walishtakiwa kwa mashitaka 12 ya uchochezi na moja la kula njama.

Mashitaka 12 yaliyokuwa yakiwakabili, katika shitaka la kula njama, wanadaiwa kati ya Februari Mosi na 16, 2018 wakiwa Kinondoni Dar es Salaam kwa pamoja walikula njama na wengine ambao hawapo mahakamani kwa kutenda kosa la jinai na kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

# Adaiwa kumuua baba kisa urithi

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

JESHI la Polisi mkoani Rukwa, linamshikilia kijana mmoja mkazi wa kijiji cha Mtenga, Nkasi mkoani Rukwa, kwa tuhuma za kumuua baba yake, Ntemi Seni (65) kwa kumkata mapanga kichwani akidai urithi wake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Justine Masejo, alisema jana kuwa, tukio la kuuawa kwa mzee huyo lilitokea Aprili 25, mwaka huu, majira ya saa 3:30 usiku katika kijiji cha Mtenga.

Alisema kijana huyo mwenye umri wa miaka 36 (jina linahifadhiwa) alikuwa akitaka baba yake ampe urithi wa mali alizonazo ili zimsaidie kuendesha maisha yake pasipo utegemezi.

Masejo alisema baada ya kijana huyo kushinikiza mara kadhaa apewe sehemu ya mali ya mzazi wake kama urithi na baba yake kukataa kufanya hivyo, kulizuka vurugu baina yao ndipo kijana huyo alipochukua panga na kuanza kumkimbiza na kisha kumkamata na kuanza kumkata kata na mapanga kichwani.


Kutokana na kitendo hicho, alisema Mzee Seni alivuja damu nyingi katika sehemu ya kichwa na kufariki dunia muda mfupi baadaye kutokana na kukosa msaada wa haraka wa kufikishwa hospitalini kwa matibabu.

Kamanda Masejo alisema mtuhumiwa huyo anashikiliwa na polisi na atafikishwa mahakamani baada ya upelelezi wa awali kukamilika.

Katika tukio lingine lililotokea Aprili 26, mwaka huu, saa 11:00 jioni katika kijiji cha Sikaunga wilayani Sumbawanga, watoto wawili ambao ni wanafunzi wa Shule ya Msingi Sikaunga, wamekutwa wamefariki dunia baada ya kuzama mtoni wakati wakiogelea.

Kamanda Masejo aliwataja wanafunzi hao kuwa ni Himid Pastor (13) mwanafunzi wa darasa la tano na Andrew Pastor (9), mwanafunzi wa darasa la pili. Wanafunzi hao, alisema walikutwa wakiwa wamefariki dunia baada ya kuzama kwenye Mto Kamawe.

Alisema miili yao imefanyiwa uchunguzi na kugundua chanzo cha vifo vyao ni kukosa hewa baada ya kuzama kwenye maji.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU
DAR ES SALAAM

SHAURI LA MADAI NO. 17 YA MWAKA 2020

M-M INDUSTRIES LTD ...MDAI

DHIDI YA

HBM IMPORT & EXPORT LTD ...MDAIWA

KWA:
The Managing Director,
HBM Import & Export Ltd,
DAR ES SALAAM

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo Mnahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au kwa Wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe 12/05/2020 saa 01.00. mchana

ANGALIA:
Kama hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama mmepokea kuitwa shaurini, itaweza kutoa hukumu kuwa mmeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 15th April, 2020 2020.

HAKIMU MKAZI MKUU
KISUTU -DAR ES SALAAM

# Selasin aanika kinachompeleka NCCR



**Na Paul Mabeja**, DODOMA

MBUNGE wa Rombo, Joseph Selasini (pichani), ametangaza kuwa ataondoka rasmi katika Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na kujiunga na NCCR-Mageuzi baada ya Bunge la 11 kufika ukomo Juni, mwaka huu.

Selasini (59), alitangaza uamuzi huo jana jijini Dodoma, alipozungumza na waandishi wa habari, akidai amekuwa akikutana na vikwazo vingi ndani ya Chadema.

Alidai kwa sasa, chama hicho kikuu cha upinzani nchini hakiendeshwi kwa misingi ya kidemokrasi kutokana na kile alichoeleza kuwa viongozi ndiyo wanapanga nani awe kiongozi na nani asiwe.

"Siku zote nilipuuza maneno na mizengwe dhidi yangu kwa kuwa niliamini ni changamoto za kisiasa. Pamoja na hayo yote, tarehe 25 mwezi huu siku ya Jumamosi, nilitolewa katika 'group' (kundi) la WhatsApp ambalo ni nyenzo muhimu ya kazi na uongozi shirikishi ndani ya chama changu bila taarifa. Hii ni sawa na kusema 'akufukuzae hakwambii toka'," alisema.

Selasini alisema kutokana na hali hiyo, aliamua kujitathimini na kuona umefika wakati sasa kwake kurudi kwenye asili yake ya uanamageuzi kwa kurejea kwenye chama chake cha zamani, NCCR-Mageuzi.

"Ukitaka kupendwa na viongozi wakuu wa chama, sharti uwe tayari kuimba kile mwandishi wa habari za kwenye mtandao ndugu Ole Mushi anakiita 'Litania ya Mwamba Tuvushe', na kwamba bila yeye huyo kiongozi, hakuna Chadema. Kwa msingi huu, hiki siyo chama cha siasa," alisema.

Alidai kuwa yeyote anayeishi nje ya wimbo huo, anachukiwa, kusimangwa na kutengwa na hivyo ndivyo alivyoishi ndani ya Chadema kwa miaka 12 ya uanachama wake.

"Nguvu ya kunivuta nirudi kwenye asili ya mageuzi ni kubwa mno, ukichanganya na msukumo wa kuikimbia Chadema, imenibidi nitumie nguvu hiyo kuwatangazia kwamba mimi Joseph Selasini nimeamua kwa hiyari yangu, siwezi kuendelea kujifunga katika kitu ambacho sikiamini," alitamba.

Aliongeza kuwa mara baada ya kumaLiza kipindi chake cha ubunge wake mwaka huu, atarejea kwenye chama alichoshiriki kukiasisi cha NCCR Mageuzi ambacho alisisitiza kuwa ndiyo baba na mratibu wa ujio wa mfumo wa vyama vingi nchini.

"Nitawaomba viongozi wa NCCR-Mageuzi waridhie na kuniruhusu kutetea jimbo langu la Rombo katika uchaguzi mkuu ujao mwaka huu kupitia NCCR-Mageuzi," alibainisha.

Bunge la 11 linatarajiwa kufungwa na Rais John Magufuli Juni 30, mwaka huu na hivyo kuhitimisha ukomo wa miaka mitano ya ubunge wa wabunge wote zaidi ya 390 walipo sasa.

HABARI KITAIFA

## Wapandishwa Kortini madai kukutwa na bangi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wawili wa Kijiji cha Mseki, Kata ya Bulungwa, Joseph Maweda (24) na Fabian Petro (20), wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, wakituhumiwa kukutwa na bangi kilo nane.

Mbele ya Hakimu mkazi wa Mahakama hiyo, Christina Chovenye, Mwendesha Mashitaka wa Polisi, Evodia Baimo, alidai kuwa wawili hao walitenda kosa hilo Aprili 21, mwaka huu, katika eneo la Mwabomba.

Alifafanua kuwa, watuhumiwa hao walitenda kosa hilo kinyume na vifungu 17(1) (b) na 2 namba 5 vya Sheria ya kuzuia na kupamba na dawa za kulevya ya mwaka vya mwaka 2017.

"Watuhumiwa hao wote kwa pamoja wamekana shitaka linalowakabili na imeahirishwa hadi Mei 25, mwaka huu itakapoanza kusikiliwa baada ya upelelezi kukamilika," alisema Baimo.

Washitakiwa wote kwa pamoja wako nje baada ya kukidhi masharti ya dhamana na kutakiwa kuwa na wadhamini wawili kila mmoja.

# GGML yatoa bil. 1.6/- kuunga mkono mapambano ya corona

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML), imetoa Sh. bilioni 1.6 kuunga mkono juhudi za Serikali kudhibiti maambukizo ya virusi vya corona ambayo hadi sasa yamesambaa katika nchi 210 duniani Tanzania ikiwamo.

Pia GGML imezindua mikakati kadhaa ya kupambana na janga la virusi hivyo vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19 katika eneo lake la kazi na kwa jamii zinazozunguka mgodi wake.

Taarifa iliyotolewa na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa GGML, Wayne Louw, imefafanua kuwa katika fedha hizo, Sh. bilioni 1.1 zitaelekezwa kwenye ngazi ya kitaifa kupitia Mfuko Maalum wa mapambano dhidi ya Covid-19 ambao unasimamiwa na ofisi ya Waziri Mkuu.

Alisema fedha zingine kiasi cha Sh. milioni 500 zitatumika kwa ajili ya kusaidia juhudi zinazofanywa katika ngazi ya mkoa na jamii, zitakazojumuisha ununuzi wa vifaatiba muhimu na vitendea kazi kama vile vifaa vya kujikinga, barakoa, mashine za kusaidia upumuaji na vingine. Aidha, alisema GGML kwa kushirikiana na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita (GEUWASA), imeweka matanki 10 ya maji yenye uwezo wa kubeba lita 1,000 kila moja kwa ajili ya kuwezesha watu kunawa mikono.

Alisema jukumu la GEUWASA litakuwa ni kujaza maji katika matangi hayo ambayo yamewekwa katika maeneo yenye watu wengi Mjini Geita.

"GGML pia itatoa dawa aina ya Chlorine ili kutakasa maji hayo, na kwa hiyo hakutakuwa na ulazima wa kutumia sabuni. Matangi mengine yanaendelea kutengenezwa kwa ajili ya Watoto na watu wenye ulemavu.

"Nia yetu ni kuendelea na shughuli zetu kama zilivyopangwa na tunatumaini kwamba janga hili litakwisha hivi karibuni. Kwetu sisi, shughuli zetu zinajumuisha uzalishaji wa dhahabu na pia utekelezaji wa miradi ya kusaidia jamii inayotuzunguka," alisema.

Naye Meneja Mwandamizi anayeshughulikia masuala ya afya mahali pa kazi, Dk. Kiva Mvungi, alisema katika kujenga uelewa juu ya janga hili kwa jamii zinazozunguka mgodi, kampuni hiyo imekuwa ikigawa vipeperushi vyenye taarifa za virusi ndani na nje ya mgodi.

"Katika kutumia vyombo vya habari kwa ajili ya uelimishaji juu ya janga la Covid-19, GGML imeingia ubia na Rubondo FM, ambacho ni kituo cha redio kinachomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Geita. Chini ya ubia huu, Kampuni ya GGML inagharimia uandaaji wa tangazo, na kituo cha Rubondo FM kitatoa mchango wake kwa kurusha tangazo hilo bila malipo.

Alisema Kituo cha Rubondo FM kilianzishwa kwa ufadhili wa GGML chini ya Mpango wa uwajibikaji kwa Jamii wa kampuni hiyo.

"Tunafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na Serikali. Maofisa wetu wawili wameteuliwa na Mkuu wa Mkoa kuwa sehemu ya kamati maalum iliyoteuliwa kupambana na janga hili hapa Geita. Wawakilishi wetu hawa wanahakikisha kwamba mipango yetu ya kupambana na Covid-19 inaendana na ile ya Serikali," alisema Dk. Mvungi.




Baadhi ya wakazi wa Mji wa Geita, wakiosha mikono kwa maji tiririka na sabuni kutoka kwenye vifaa vilivyotolewa na kampuni ya GGML. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Awamu ya mwisho uboreshaji daftari wapigakura mwezi ujao

**Na Elizabeth Zaya**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) inatarajia kuanza awamu ya pili ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura kuanzia Mei 2 mwaka huu katika mikoa kadhaa.

Akizungumza na Nipashe, Kaimu Mkurugenzi wa NEC, Gerald Mwanilwa, alisema awamu ya pili ilianza Aprili 17 hadi 19 mwaka huu.

Alisema mikoa ambayo tayari wamekwishamaliza kazi hiyo ni pamoja na Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Mara, Simiyu, Mwanza, Shinyanga, Geita, Kagera, Kigoma na Tabora.

Mwanilwa alisema Mei 2 wataanza uboreshaji huo wa daftari la wapigakura katika mikoa mingine ya Zanzibar na Tanzania Bara.

Alitaja baadhi ya mikoa ambayo itahusishwa katika kazi hiyo kwa Tanzania Bara kuwa ni pamoja na Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Mtwara, Lindi, Ruvuma, Njombe, Songwe, Iringa, Dodoma, Singida, Rukwa na Katavi.

"Tunafanya kazi hii kwa tahadhari kubwa sana na tumezingatia ushauri uliotolewa na wataalam wa afya katika kufanya kazi hii.

"Hatujapata tatizo la watu kutokujitokeza, lakini tunatekeleza kazi hii katika kipindi hiki cha tishio la ugonjwa wa corona kwa kuzingatia ushauri tuliopewa ikiwamo kuhakikisha hatuweki msongamano wa watu, tunahakikisha wanakaa kwa umbali sana.

"Katika vituo vyote vinavyofanya kazi hii, tumejitahidi kuweka maji tiririka na sabuni pamoja na vitakasa mikono," alisema.

Mwanilwa alisema tayari maandalizi yote kwa ajili ya kazi hiyo kwa mikoa inayofuata yamekamilika na vifaa vyote vimepelekwa katika maeneo husika.

Pia alisema kazi hiyo ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura inaenda pamoja na uwekaji wazi wa daftari hilo.

"Tunaboresha daftari, lakini pia kazi hiyo inaenda pamoja na uwekaji wazi wa daftari hilo la kudumu la wapiga kura.

"Lengo kubwa tunataka kila mwenye pingamizi afike na kuleta malalamiko yake ili yapitiwe na kufanyiwa kazi.

"Kwa hiyo tunawaomba wananchi katika mikoa hii tuliyoitaja wajitokeze kuboresha taarifa zao, na wakumbuke kwamba hii ndiyo mara ya mwisho, hivyo ni muhimu wakaboresha ili wasikose haki yao ya msingi ya kupiga kura."

# Serikali yaahidi neema upanuzi wa hospitali

SERIKALI imeanza kuipanua Hospitali ya Wilaya ya Kahama kwa kujenga jengo la kisasa la wagonjwa wa nje ambalo litakamilika Julai mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa bungeni jana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), ilipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Azza Hamad.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema Hospitali ya Wilaya ya Kahama ina msongamano mkubwa wa wagonjwa.

"Je, ni linì serikali itatenga fedha za kutosha ili kuongeza miundombinu katika hospitali hiyo?" alihoji.

Katika majibu yake, Tamisemi ilisema Serikali imeanza kuipanua na upanuzi huo utakamilika Julai mwaka huu. Ilisema usanifu wa jengo la ghorofa mbili la huduma ya afya ya mama na mtoto tayari umekamilika.

"Ujenzi utaanza katika mwaka wa fedha 2020/21, jengo hilo likikamilika, litakuwa na vitanda 320 ambavyo vitasaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama kwa kiasi kikubwa," ilisema.

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Kuteuliwa, Anne Malecela (pichani), amesema takwimu zinaonyesha kuwa huduma za afya hazifanani na haziko sawa mkoa kwa mkoa, wilaya kwa wilaya na hata vijiji kwa vijiji.

"Je, serikali inafanya jitihada gani ili kuondoa hali hiyo ili watu wa mikoa yote, wilaya zote, mijini na vijijini wapate fursa sawa ya huduma ya afya?" alihoji.

Katika majibu yaliyotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwa swali hilo, ilielezwa kuwa serikali inaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya katika maeneo yote nchini, ili kuhakikisha huduma hizo zinapatikana kwa uwiano kwa wananchi wote.



Wizara hiyo ilisema Sera ya Afya ya Mwaka 2007 inaelekeza kuwa huduma za afya zitatolewa kwa kuzingatia uwiano wa kijiografia, mzigo wa magonjwa na idadi ya watu.


Ilisema katika kutimiza azma hiyo, serikali imeboresha au kujenga vituo vya afya 352, hospitali za rufani za wilaya 67 na hospitali za rufani za mikoa tano katika mikoa mipya mitano ya Songwe, Katavi, Simiyu, Njombe na Geita, ili kuhakikisha huduma bora na za kibingwa zinawafikia wananchi kwa ujumla.

# Mfuko wa Barabara waongezewa fedha

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imesema katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2015 hadi 2020, umeongezewa fedha kutoka Sh. bilioni 218.55 hadi Sh. bilioni 251.73.

Hayo yalielezwa jana bungeni na ofisi hiyo ilipojibu swali la Mbunge wa Moshi Mjini (Chadema), Japhary Michael (pichani).

Mbunge huyo alisema utendaji wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (Tarura) katika Manispaa ya Moshi unakabiliwa na tatizo kubwa la upungufu wa fedha kiasi na kusababisha manispaa kuwa na barabara mbaya kuliko hata zilipokuwa zikisimamiwa na halmashauri.




**Habari zote na Augusta Njoji,**
DODOMA



"Je, serikali haioni haja ya kuongeza bajeti ya Tarura ili iweze kukabiliana na changamoto ya uharibifu wa barabara katika Manispaa ya Moshi? Je, ni lini serikali itafanya tathmini ya mafanikio na changamoto za Tarura, ili kuona namna ya kuifanyia maboresho?" alihoji.

Katika majibu yake kwa mbunge huyo, ofisi hiyo ilisema kuna ongezeko la Sh. bilioni 33.18.

"Katika mwaka wa fedha 2020/21, fedha za Mfuko wa Barabara zimeongezeka na kufikia Sh. bilioni 275.03 ambapo kipaumbele cha matumizi ya fedha hizo kitakuwa ni uboreshaji wa miundombinu iliyoharibiwa na mvua inayoendelea kunyesha nchini," ilisema.

Ofisi hiyo pia ilisema serikali itatafuta fedha kutoka vyanzo vingine kwa ajili ya matengenezo ya dharura ya barabara za vijijini na mijini zilizoharibiwa na mvua.

# Wizara yasaka mtaalamu vyanzo mbadala vya maji

WIZARA ya Maji kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro, imeanza mchakato wa kumtafuta mtaalam mshauri atakayefanya utafiti wa vyanzo mbadala vya maji katika Manispaa ya Morogoro.

Hayo yalibainishwa jana na wizara hiyo ilipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Jasmine Bunga (pichani).

Katika swali lake, mbunge alisema mito mingi na chemchem zinazopeleka maji katika Bwala la Mindu, hukauka wakati wa kiangazi kutokana na mabadiliko ya tabianchi na kusababisha kiwango cha maji kushuka, hivyo wananchi wa Manispaa ya Morogoro kupata adha.

"Je, serikali haioni kuna haja ya kutumia Mto Mgeta uliopo Tarafa ya Mgeta, Mvomero kusambaza maji katika Manispaa ya Morogoro?" mbunge alihoji.

Katika majibu yake kwa mbunge huyo, wizara hiyo ilisema upungufu wa maji kwa mito inayotiririsha maji kuingiza Bwawa la Mindu pamoja na mabadiliko ya tabianchi, unasababishwa na shughuli za kibinadamu kwenye Mlima Uluguru ambazo zinahitaji jitihada za pamoja ili kulinda uendelevu wa Bwawa hilo muhimu.

Katika kukabiliana na tatizo hilo, wizara ilisema imeanza mchakato huo na kazi hiyo inatarajiwa kuanza mapema mwaka wa fedha 2020/21 kwa kutumia fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ya Ufaransa (AFD).

"Mkataba wa fedha unatarajiwa kutiwa saini mwishoni mwa mwaka wa fedha 2019/20. Utafiti utakapokamilika, utaonyesha uwezekano wa kutumia Mto Mgeta na vyanzo vingine kwa ajili ya Manispaa ya Morogoro na maeneo ya njiani ili kuhakikisha mizania ya maji inakuwa endelevu," ilisema.







# ‘Elimu kubaini bidhaa bandia itolewe vijijini’

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAJUMBE wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, wametaka elimu ya uhakiki wa stempu za kielektroniki (ETS), kuwafikia wananchi wa vijijini ili kuwa na uelewa wa kubaini bidhaa feki.

Ushauri huo ulitolewa juzi na wajumbe hao kwenye semina ya kamati hiyo na Kampuni ya Societe Industrielle de Produits Alimentaire (SICPA) ya Uswisi, iliyoingia ubia na Mamlaka ya Mapato (TRA) kuanzisha mfumo wa ETS ambao umesaidia kuokoa upotevu wa mapato ya serikali.

Akichangia katika semina hiyo, mjumbe wa kamati hiyo na Mbunge wa Kigoma Kusini (CCM), Hasna Mwilima, alisema elimu hiyo inatakiwa pia kuwafikia wananchi wa vijijini ili kubaini bidhaa feki ambazo hazina stempu hizo.

Mbunge wa Bariadi (CCM), Andrew Chenge, alipongeza mfumo huo kwa kusaidia kudhibiti mapato ya nchi.

“Hivi ni kwanini nchi za jirani kama Kenya na Uganda hazitumii mfumo huu na hapa tunaona mfano uliotolewa ni wa nchi zingine nje ya Bara la Afrika?” Chenge alihoji.

Awali, akiwasilisha mada kwa kamati hiyo, Meneja Mkuu wa SICPA kwa upande wa Tanzania, Xavier Davard, alisema mfumo huo licha ya kuokoa upotevu wa mapato ya serikali, pia umedhibiti ufanyaji wa biashara haramu na namna ya kubaini bidhaa feki.

Alisema mfumo huo kwa sasa umeanza kwenye bidhaa za pombe na hatua ya pili ni vinywaji baridi kama maji na soda.

“Kwa sasa, bado tunafanya utafiti kwenye viwanda vya bidhaa za mafuta na saruji,” alisema.

Aliongeza kuwa nchi jirani na Tanzania ziko kwenye mchakato wa kutumia mfumo huo, akibainisha kuwa Kenya wataanza na bidhaa za pipi na chokleti.

“Matumizi ya stempu za kielektroniki za kodi kwa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa yalianzishwa kuchukua nafasi ya matumizi stempu za karatasi ambazo matumizi yake yalihusishwa na vitendo vya ukwepaji kodi pamoja na bidhaa bandia kwa kiasi kikubwa,” alisema.



Mchuuzi wa biashara ndogo ambaye jina lake halikupatikana, akitafuta wateja wa barakoa na biashara ya mabegi katika Barabara ya Tabora jijini Dodoma jana. Uwapo wa ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona, umetoa fursa kwa kundi hilo la wajasiriamali kuchangamkia soko la barakoa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ataka makundi maalum yakumbukwe Ramadhani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa Halmashauri Kuu ya Baraza la Waislamu, Wilaya ya Dodoma, Alhaji Bashuru Hussein, amewataka waumini wa dini hiyo kuyasaidia makundi maalum, wakiwamo wazee, ili kupunguza makali ya mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Hussein alisema wazee, wajane na watoto yatima wanahitaji kusaidiwa, ili kutimiza vyema mfungo wao kwa kuwa hawana uwezo.

“Mwezi huu wa Ramadhani ni wa pekee kwa kila mwaka, ni mwezi wa ibada na wakifanyiwa hivyo kwa waumini wasiojiweza watakuwa wametimiza pia tendo la kutoa sadaka,” alisema.

Akizungumzia mapambano dhidi ya maambukizo ya ugonjwa wa corona, alisema katika kipindi hiki, ni vizuri waumini wakatii maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya na viongozi wa serikali na dini.

Aliwataka waumini kuacha tabia ya kulala misikitini na kutofanya mikusanyiko pindi wanapomaliza sala kutokana na ugonjwa huo.

“Kipindi hiki tunakabiliana na ugonjwa wa corona, ni muhimu tukabadilika na tukaacha mazoea ili kujilinda sisi wenyewe na janga hili,” alisema.

Alisisitiza viongozi ndani ya misikiti kuendelea kutoa elimu kwa waumini wao kwa vitendo ili kuwanusuru na maambukizo ya ugonjwa huo.

# Mradi maalum wa utafiti malisho mifugo waanza

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Kituo cha Hombolo kwa kushirikiana na Shirika la Advanta Seed International, wameanza kutekeleza mradi maalum wa kutafiti na kuzalisha mbegu bora za malisho ya mifugo.

Akizungumza na Nipashe katika ziara maalum ya kutembelea mashamba ya utafiti wa mbegu hizo, Mzalishaji Mbegu Mkuu wa Kituo hicho, Dk. Lameck Nyaligwa, alisema mradi huo wa mwaka mmoja utafanya utafiti wa mbegu hizo kwenye mazao ya mtama na uwele.

Alisema mradi huo unatarajia kuleta mapinduzi makubwa katika sekta ya mifugo nchini.

Alizitaja aina za mbegu za mtama ambazo zipo katika mashamba hayo ya majaribio kuwa ni Sugar - Grace, Mega-Sweet, BMR Rocket na Jumbo-Gold.

“Mbegu hizi zinazalisha majani na miti yenye virutubisho muhimu sana kwa ajili ya malisho ya wanyama, hususan katika kuongeza uzito wa mnyama pamoja na uzalishaji wa maziwa,” alisema.

Pamoja na hayo, alisema mradi huo utakapopitishwa na wataalamu, utaongeza fursa za kiuchumi miongoni wa wakulima, wafanyabiashara na wafugaji.

“Mradi huu utakapopitishwa, utatoa fursa kwa wakulima kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania kuja kununua mbegu husika na kwenda kuzalisha malisho haya ya kisasa na kuyauza kwa wafugaji, hali ambayo itawaongezea kipato,” alisema.

Dk. Nyaligwa alisema kituo kitafungua milango kwa kampuni kubwa nchini kwenda kununua mbegu hizo kwa ajili ya kulima katika mashamba makubwa na baadaye kuyasindika majani hayo ili kuyauza katika maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi.

Diwani wa Hombolo Bwawani, Ased Ndajilo, alisema mradi huo unatarajiwa kuleta mapinduzi makubwa kwa wafugaji na wakulima nchini.

Aliwataka wafugaji na wakulima wote nchini kuchangamkia fursa hiyo muhimu, mara tu mradi huo utakapopitishwa na wataalamu husika.

Monica Malundo, mkazi wa kata hiyo, alisema mfumo wa mazao ya malisho utapunguza kasi ya ufugaji wa kuhamahama kwa ajili ya kutafuta malisho.

Alisema wafugaji wengi wamekuwa wakilisha mifugo yao kwa kutafuta malisho, hivyo kutokana na utafiti uliofanywa na TARI-Hombolo kubaini mazao bora ya malisho, utakuwa mkombozi mkubwa kwa wafugaji na watakuwa wanafuga kwa tija.



# H'shauri kuweka mashine kunawia maeneo muhimu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya imesema itanunua mashine tano za kunawia mikono ambazo zitawekwa kwenye maeneo muhimu ya kutolewa huduma ikiwamo hospitali na stendi kuu ya mabasi kukabiliana na maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa corona.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Jiji hilo, Kamishna msaidizi wa Polisi, James Kasusura alipokuwa akizungumza na Nipashe juu ya hatua wanazoendelea kuzichukua katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Covid-19.

Kasusura alisema mashine hizo zitafanya kazi bila mtu kugusa koki na kusaidia kupunguza maambukizo kwa wengine ikilinganishwa na ilivyo sasa.

"Mashine hizo zinatengenezwa na Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (Must), chuo hicho tayari kilianza kusambaza mashine hizo maeneo mbalimbali na tayari Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, iliagiza kila ofisi ya umma inunue mashine hizo," alisema Kasusura.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alisisitiza wananchi kuendelea kunawa mikono mara kwa mara kwa sababu ugonjwa wa Covid-19 tayari umeanza kuenea maeneo mbalimbali.

Alisema njia pekee ya kukabiliana na ugonjwa huo ni kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni pamoja na kujifukiza kwa kutumia mimea ambayo imeshauriwa.

Mwenyekiti wa stendi kuu ya mabasi mkoani humo, Salum Hashimu, aliishukuru serikali kwa kuwa mstari wa mbele dhidi ya mapambano ya vita ya ugonjwa wa Covid-19 kwa kutoa elimu pamoja na vifaa vya kujikinga ikiwamo mashine.

Alisema maofisa wasafirishaji (wapiga debe), wameanza utaratibu kwa kuhakikisha kila ofisi ya basi inakuwa na ndoo za maji pamoja na sabuni na siyekuwa navyo anatozwa faini, lakini pia kila abiria anayeingia sharti anawe mikono.

# Takukuru yaokoa mil. 300/- kutokana na ubadhirifu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Mkoa wa Mbeya, imeokoa zaidi ya Sh. milioni 300 kutoka vyama vya msingi vya wakulima na vyama vya akiba na mikopo baada ya kubaini ubadhirifu.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake juzi, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi alisema, fedha hizo zilipatikana baada ya kufanya ufuatiliaji kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi, mwaka huu.

Alisema Takukuru ilibaini ubadhirifu huo kwenye vyama vya msingi vya wakulima na vyama vya akiba na mikopo kutoka taasisi mbalimbali ambao ulifanywa na viongozi wa vyama hivyo.

"Tulifanya uchunguzi kwenye vyama 20 kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya usalama kutoka maeneo mbalimbali ya mkoa huo na kufanikiwa kuokoa kiasi cha Sh. milioni 300 ambazo tayari ziliwekwa kwenye akaunti binafsi za watendaji wa vyama hivyo," alisema Matechi.

Alibainisha mchanganuo wa mahali fedha hizo zilikusanywa kuwa ni Sh. milioni 57 kutoka wilaya ya Mbarali, Rungwe milioni 33 , Kyela milioni 35 na Chunya milioni 11.

Alisema baada ya kubaini ubadhirifu huo Takukuru kwa kushirikiana na watendaji wa vyama hivyo pamoja na Mrajisi wao walihakikisha fedha hizo zinarejeshwa huku akibainisha lengo la kuwashirikisha ni kuhakikisha changamoto hizo hazijirudii tena. Aliongeza kuwa katika kipindi cha robo ya mwaka kuanzia Januari hadi Machi 2020, Takukuru ilipokea jumla ya tuhuma 121 zinazohusiana na masuala ya rushwa. Alisema tuhuma hizo za rushwa zinatoka katika taasisi mbalimbali za umma ikiwamo Jeshi la Polisi, Mahakama, Hospitali na Idara ya Maji pamoja na taasisi binafsi.

Matechi aliwashauri watumishi wote wa umma kuzingatia kanuni na taratibu za kazi katika kutimiza wajibu wao ili kuepukana na vitendo vya rushwa.



Mtafiti wa Matunda kutoka Taasisi ya Kilimo Tanzania Tari, Kituo cha Uyole, Daud Mbongo, akitoa elimu ya shamba darasa kwa wakulima (hawapo pichani) kuhusu aina mbalimbali za mbegu ya mparachichi walizozitafiti ili zitumike kulingana na maeneo husika .**PICHA NA GRACE MWAKALINGA**

# Watakiwa kudhibiti watoto wa kike

**Na Grace Mwakalinga,**

MBEYA

WAZAZI na walezi mkoani Mbeya wameshauriwa kuwadhibiti watoto wao hususani wa kike kwa kuhakikisha hawafanyiwi vitendo vya ukatili wa kijinsia kama ubakaji kipindi hiki ambacho shule zimefungwa ili kudhibiti maambukizo ya ugonjwa wa Covid-19.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mwenyekiti wa Vituo vya Taarifa na Maarifa wilayani Mbeya, Flora Mlowezi, ambaye alisema kipindi hiki ni muhimu wazazi wakachukua tahadhari kuwalinda watoto wa kike dhidi na vitendo vya ubakaji.

Alisema wakati huu familia zikiwa nyumbani ni vyema mabinti wakawekewa tahadhari kubwa ikiwamo kutoruhusu ukaribu na wanaume wanapofanya kazi za nyumbani au mama anapokuwa sokoni.

Alisema idadi kubwa ya wanaofanya vitendo vya ubakaji ni ndugu wa karibu katika familia hivyo ni wakati wa kuwa makini.

"Kipindi hiki watoto wakiwa nyumbani tunahitaji kuwa waangalifu sana na usalama wao hasa mabinti zetu hawa maana baadhi ya wanaume wanawamezea mate wakitamani kuwabaka, tukiruhusu haya itakuwa hatari zaidi maana ni muda wa kukabiliana na corona," alisema Mlowezi.

Mkuu wa Dawati la Jinsia mkoani humo, Janeth Masangano, aliapa kuwachukulia hatua wote watakaowafanyia vitendo vya ukatili watoto wa kike.

Alisema kipindi hiki shule zimefungwa watoto wanatakiwa kuwekwa kwenye uangalizi maalum kwa kuhakikisha hawanasi kwenye mitego ya mafataki.

Aliwaomba wazazi husasani kinamama ambao ni wafanyabiashara kabla ya kwenda kwenye majukumu yao wahakikishe mabinti wanakuwa salama.

Katika kuhakikisha watoto na wanawake wanakuwa salama kipindi hiki cha mapambano dhidi ya ugonjwa wa Covid-19, Mkurugenzi wa Mtandao wa Jinsia nchini TGNP- Mtandao, Lilian Liundi alishauri mambo ya kukabiliana na vitendo vya ukatili.



# Waliopona corona walalamikia kunyanyapaliwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BAADHI ya wagonjwa waliopona ugonjwa wa corona na kuruhusiwa kurudi katika familia zao, wamelalamikia kitendo cha kunyanyapaliwa na jamii.

Wakizungumza na mwandishi wetu, walisema bado jamii haijaamini kuwa wameshapona ugonjwa huo hivyo kukosa ushirikiano.

Fatma Juma (si jina halisi), ambae amepona na kuruhusiwa kutoka hospitali, alisema baada ya kufika nyumbani kwake, alikutana na hali ya unyanyapaa kwa wapangaji wezake.

Alieleza baada kungia ndani ya nyumba akiwa amevaa barakoa, wapangaji wezake wakaanza kumkimbia na kumshangaa, wakiamini kuwa ametoroka katika kambi ya wagonjwa wa corona. "Niliwaeleza kuwa mimi tayari nimeshapona na nimeruhusiwa kurudi nyumbani, lakini walishindwa kuniamini na kuanza kunikimbia," alisema.

Alieleza kuwa ameamua kujifungia chumbani kwake na kufuata maelekezo ya watalamu wa afya aliyopewa ya kutojichanganya na watu kwa siku 14.

Halima Ali ambae sio jina lake halisi, pia ni miongoni mwa wagonjwa waliopona corona, alisema baada ya kufika mtaani kwao, baadhi ya majirani zake walianza kuchungulia madirishani, huku wakiwa hawaamini kama ameshapona.

"Wakati nateremka katika gari la wagonjwa (ambulance), baadhi ya majirani walianza kuchungulia madirishani, huku wakisema kuwa corona hiyoo," alisimulia.

Alieleza kuwa wakati akiwa bado hospitali akipata matibabu, shemeji yake ambae anaishi nae alikuwa akitengwa na baadhi ya wanajamii.

Alisema wakazi wa kijiji anachoishi wamekuwa wakiinyooeshea vidole nyumba yao na kusema kuwa wasiikaribie kwa sababu imetoka mgonjwa wa corona.

Alieleza kuwa bado jamii haina uwelewa kuwa corona unatibika na wao wana imani kuwa ukipata corona ndo umekutwa na mauti. Mmoja ya muhudumu wa Wizara ya Afya ambae hakutaka kutajwa jina lake, alisema baadhi ya wagonjwa wa corona waliopona wamekataliwa na familia zao wakihofia kuwa bado wataambukizwa virusi.

"Juzi wakati tunawarejesha wagonjwa waliopona, kuna familia moja ilimkataa ndugu yao ambae ameshapona na hana maambukizo, ilitulazimu tutoe elimu kwa familia hiyo na baadae iliridhika na kumpokea," alisema. Alieleza hali ya unyanyapaa kwa jamii kwa waliopona corona ni kubwa sana kwa kuwa hata mitaani wanapoiona gari la Ambulence, wanaikimbia wakiamini kuwa ina wagonjwa wa corona.

"Unafika katika mitaa kwa ajili ya kuwafuata wagonjwa au kuwarejesha waliopona au kuwafuata wale wenye dalili za corona kuwafanyia vipimo, unakuta kundi kubwa la watu wapo nje ya nyumba ambayo ina mgonjwa, na wakati mwengine hata kabla majibu hajatoka, wanavumisha kuwa mgonjwa huyo ana corona," alisema.

Wziri wa Afya, Hamad Rashid Muhammed, alisema unyanyapaa kwa wagonjwa wa corona na waliopona ugonjwa huo ni mkubwa sana katika jamii.

Alitaka jamii kufahamu kuwa mgonjwa wa corona ni sawa na mgonjwa mwingine, anapotoka hospitali anatakiwa kupewa ushirikiano, hivyo hakuna haja ya kuwanyanyapaa.

Alieleza kuwa jambo la muhimu kila mmoja kuchukua tahadhari na kufuata maelekezo ya watalamu wa afya ikiwamo kuvaa barakoa na kutokaa katika mikusanyiko hadi hapo hali itakapokuwa shwari.



Kinamama katika Soko Kuu la Darajani Mjini Zanzibar, wakiwa katika biashara ya samaki, licha ya uhaba uliopo hivi sasa wa kitoweo hicho. **PICHA: MARTIN KABEMBEA.**

# Wazanzibari wote watakiwa kuvaa barakoa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema wakati umefika sasa kwa kila mwanajamii kujenga utamaduni wa kuvaa barakoa ili kujiepusha maambukizo ya virusi vya corona.

Alisema taifa bado liko katika kipindi kigumu, kutokana na wimbi la maambukizo ya virusi hivyo, ambavyo vinazunguuka mitaani baada ya Serikali kufanikiwa kuzuia maambukizo kutoka nje ya nchi.

Balozi Iddi aliyasema hayo ofisini kwake Vuga Mjini Zanzibar baada ya kupokea msaada wa mashuka 20 na mashine 30 za kupimia joto la mwili zilizotolewa na mfanyabiashara maarufu, Said Nasser Nassor (Bopar), akikamilisha msaada aliyoahidi kutoa katika kuunga mkoni jitihada za Serikali kwenye mapambano dhidi ya virusi vya corona.

Balozi Iddi, alisema ugonjwa wa mafua na homa kali ya mapafu inayosababishwa kupumua kwa shida pamoja na kikohozi kutokana na virusi hatari vya corona umo ndani ya jamii ukisambaa, jambo ambalo linahitaji kuchukuliwa kwa tahadhari kubwa.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inahamasisha viwanda vidogo kutengeneza barakoa ili kuwapunguzia gharama kubwa wananchi hasa wale wa kipato cha chini wanaolazimika kununua vifaa hivyo kutoka nje ya Nchi kwa bei ya juu.

Makamu wa Pili wa Rais alimpongeza na kumshukuru mfanyabiashara huyo kwa uzalendo wake wa kujitolea kusaidia jamii inapopata changamoto.

Aliwakumbusha wananchi kutoona shinda kuendelea kutumia dawa za asili kama nyungu na vyakula vyenye asili ya ukali (itamin C) ambavyo kwa mujibu wa wataalamu wa afya, ni rahisi kusaidia kuongeza kinga mwilini.

Naye mfanyabiashara Bopar, alisema yuko tayari kusaidia jamii na Serikali pale linapotokea suala la dharura kwa jamii.

Bopar alisema yeye kama Mzanzibari na mzalendo wa Taifa hili, hana sababu ya kutoiunga mkono Serikali pale inapotokea dharura au kuombwa kufanya hivyo wa maslahi ya Taifa na wananchi wake.

# Mama wa mtoto aliyedhalilishwa apata matumaini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMA wa mtoto aliyedhalilishwa kwa kubakwa na kulawitiwa, amesema ana matumaini makubwa ya kupata haki kutokana na mwenendo wa kesi hiyo unavyokwenda.

Kesi hiyo namba IR 64/2020, inamhusisha mwanamume mwenye umri wa miaka 40 ambae anadaiwa kumbaka mtoto wa miaka 11 huko Dole Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja wa Disemba Mosi, mwaka jana.

Akizungumza na Nipashe, mama huyo (jina lake limehifandhiwa), alisema kesi hiyo ipo katika Mahakama ya Mkoa Vuga, na inatarajiwa kuendelea leo.

Alisema kuwa kesi imeshindwa kusikilizwa kutokana na uwapo wa maradhi ya Covid-19, lakini alisema anaamini baada ya kumalizika kwa ugonjwa huo, itakwenda vizuri.

"Nalipongeza sana Jeshi la Polisi kuharakisha uchunguzi wa kesi yangu, na mshitakiwa kufikishwa mahakamani,"alisema mama huyo.

Alieleza kuwa alimgundua mtoto wake baada ya kumuona hawezi kukaa vizuri, na ndipo akipoanza kumchunguza na kumpeleka hospitali, ambapo daktari alithibitisha kuwa amebakwa na kulawitiwa.

Aidha alisema mtoto wake alipohojiwa, alimtaja aliemfanyia kitendo hicho, na hatua za kisheria zikaanza kuchukuliwa na mtuhumiwa yupo rumande.

"Nashukuru nilipotakiwa kupeleka mashahidi mahakamani nimepata ushirikiano wa watu kwenda kutoa ushahidi kwa sababu baadhi ya majirani zangu walikuwa wakimuona mtuhumiwa akimpa pesa mtoto wangu," alisema.

Alieleza kuwa ana imani kwamba maradhi ya corona yatakapoisha kesi hiyo itaweza kuendelea kusikilizwa na kutolewa hukumu inayostahiki.

Naye Mratibu wa Shehia ya Dole, Salama Masanja, alisema kesi hiyo imemsikitisha sana kutokana na umri mdogo wa mtoto huyo ambae alibakwa na kulatiwa.

Alieleza kuwa yupo pamoja na familia ya mtoto huyo ili kuhakikisha haki inapatikanai.

Sheha wa Shehia ya Dole, Hamdu Juma Majengo, aliwataka wakazi wa shehia hiyo kutowafumbia macho watuhumiwa wala kuwaonea huruma kwa sababu vitendo wanavyovifanya ni kinyume cha haki za binadamu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NAFASI ZA KAZI**

WANAHITAJIKA FULL TIME PHARMACEUTICAL ASSISTANTS NA PHARMACY DISPENSERS. **CONTACT: 0755 903874 / 0754 275627.**

## NIPASHE NI JIBU LAKO

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SALMA MUSTAFA MLANDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 572 DPM TOYOTA SIENTA.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/339193/2020.**

115720802

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ERASTO BENEDICT MARO** anatangazakupotelewanakadiyagariyenyenambazausajiliT501 DPS Chassis namba **AFATXXM12TBY16869** Engine namba **WLAT 1277554.** Yeyoteatakayeionaatoetaarifakituo cha polisi.Taarifayapolisi: **DOD/DOD/RB/343232/2020.**

215720702

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA**

**Probate and Administration cause No...... Of 2020**

**In the matter of the estate of the late signed at Dodoma by**

**ELIAS JOSEPH MZENGA of KIZOTA MBUYUNI within Dodoma City**

**AND**

**In the matter of application for letters of administration by**

**MONICA EDWARD MZENGA**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules GN. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 25th day of May, 2020.

Dated at Dodoma this 28th day of April, 2020

RESIDENT MAGISTRATE

215720002

**Uza,**

**Chenye**

**Thamani Kubwa Kwa**

**Kutangaza Nasi**

**Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Uamuzi kesi ya Mdee Mei 28

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imesema itatoa uamuzi wa kama Mbunge wa Kawe, Halima Mdee anayekabiliwa na kesi ya uchochezi ana kesi ya kujibu au la Mei 28, mwaka huu.

Kesi hiyo ilipangwa kutolewa uamuzi huo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba baada ya upande wa Jamhuri kufunga ushahidi wao.

Hata hivyo, mdhamini Martha Mtiko, alidai kuwa mshitakiwa ameshindwa kuja mahakamani kwa sababu ni mgonjwa.

"Mheshimiwa hakimu mimi ni mdhamini wa Mdee ameshindwa kuja mahakamani leo afya yake si nzuri anaumwa," alidai Mtiko.

Awali, Wakili wa Serikali Silvia Mitanto, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kusikilizwa uamuzi wa kama mshitakiwa ana kesi ya kujibu au la, lakini mshtakiwa hayupo mahakamani.

Hakimu alisema kwa kuwa mshitakiwa ni mgonjwa mahakama yake itatoa uamuzi Mei 28, mwaka huu dhidi ya kigogo huyo wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Taifa.

Mapema mahakamani hapo akifunga ushahidi wa Jamhuri, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kwamba mashahidi watatu wanatosha kujenga kesi yao dhidi ya mshitakiwa.

Mapema mahakamani hapo, mashahidi watatu wa upande wa Jamhuri wametoa ushahidi akiwamo Mkuu wa Kituo cha Polisi cha Urafiki, Mrakibu wa Polisi (SP) Batseba Kasanga.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa Julai 3, 2017 katika Makao Makuu ya Ofisi ya Chadema iliyopo mtaa wa Ufipa Wilaya ya Kinondoni, Mdee anadaiwa kutamka maneno dhidi ya Rais John Magufuli kuwa "anaongea ovyo ovyo, anatakiwa afungwe breki" na kwamba kitendo hicho kingeweza kusababisha uvunjifu wa amani.

Mdee alifikishwa mahakamani hapo kwa mara ya kwanza na kusomewa mashitaka yake Julai 10, 2017 na yupo nje kwa dhamana.




Mshindi wa mwezi Machi wa shindano la TUSUA MAPENE NA VODACOM, Sharabi Myovela( mwenye fulana nyekundu), mkazi wa Iringa, akiwa na familia yake baada ya kukabidhiwa mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 10 toka kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania PLC. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mtumishi mahakama kortini tuhuma za kuomba rushwa

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MSAIDIZI Mkuu wa Ofisi ya Mahakama ya Mwanzo Mwandiga, Jackson Mrefu, amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kigoma kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 170,000.

Mrefu alifikishwa mahakamani hapo jana saa 3:00 asubuhi na kupandishwa kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Gadiel Mariki na kusomewa mashitaka ambayo alikana.

Kwa sasa yuko nje kwa dhamana ya mdhamini mmoja mwenye barua ya utambulisho kutoka kwa ofisa mtendaji wa kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni mbili.

Upande wa Mashitaka ukiongozwa na Mwendesha Mashitaka wa Taaasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Kigoma, Boniface Kamwesigile, ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kumsomea mshitakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Mariki alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Mei 28, mwaka huu.

Kamwesigile alidai mashitakiwa alitenda kosa la kwanza Septemba 19, mwaka jana, akiwa Mahakama ya Mwanzo Mwandiga kwa kuomba rushwa ya Sh. 170,000 kutoka kwa Imelda Dosha kama sharti ili kumfungulia kesi ya Madai namba 45/2019 katika mahakama hiyo.

Alidai kuwa mshitakiwa alitenda kosa la pili Septemba 19, mwaka jana, akiwa Mahakama ya Mwanzo Mwandiga kwa kupokea Sh. 30,000 kutoka kwa Imelda Dosha kama sharti ili kumfungulia kesi hiyo.

Kamwesigile pia alidai kuwa mshitakiwa alitenda kosa la tatu Septemba 20, mwaka jana, akiwa mahakamani hapo kwa kupokea Sh. 60,000 kutoka kwa Imelda Dosha ili amfungulie kesi.

Alidai kuwa mshitakiwa huyo alitenda kosa la nne Septemba 25, mwaka jana, mahakamani hapo kwa kupokea Sh. 70,000 kutoka kwa Imelda Dosha ikiwa ni sharti la kumsaidia kufungua kesi aliyokuwa amekusudia kuifungua.

Pia alidai kuwa mshitakiwa alitenda kosa la tano Septemba 26, akiwa mahakamani hapo kwa kupokea Sh. 10,000 kutoka kwa Imelda Dosha kwa njia ya M-Pesa kama sharti ili kumfungulia kesi hiyo ya madai.

## Kundi la tembo lamuua mkulima

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MKAZI wa kijiji cha Angalia, Tunduru mkoani Ruvuma, Rajab Kapilipili (43), amefariki dunia baada ya kushambuliwa na kundi la tembo.

Taarifa za tukio hilo zinaeleza kuwa, Kapilipili alikubwa na mkasa huo wakati akijaribu kuwafukuza tembo hao ambao walivamia shamba lake.

Mashuhuda wa tukio hilo walisema jana kuwa Kapilipili alikanyagwa kanyangwa na kupasuka na kuvunjika viungo vya sehemu mbalimbali za mwili wake na kusababisha kifo chake.

Walisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 2.00 usiku katika kijiji cha Chikunja eneo la Mto Mwambesi.

Kaimu Ofisa Wanyamapori wa Wilaya ya Tunduru, Ally Limbega, amekiriki kuwapo kwa tukio hilo na kwamba tayari amepeleka askari wa idara hiyo kwa ajili ya kuwafukuza tembo hao ili wasiendelee kuleta madhara.

Aidha, Limbega amewataka wananchi wanaoishi katika maeneo yenye wanyama kuwa na tahadhari ili kujiepusha ma matukio hayo.

Kamanda wa Polis Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, amethibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kwamba polisi wanaendelea na uchunguzi.

## Wazawa kupewa kipaumbele uanzishaji bucha nyamapori

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

SERIKALI imesema Watanzania watapewa kipaumbele katika kuendesha biashara ya nyama za pori kwenye bucha kwa lengo la kuwawezesha kujiongezea kipato na ajira.

Kutokana na azma hiyo, serikali imesema ni muda mwafaka kwa kila Mtanzania kuchangamkia maombi ya leseni za biashara hiyo inayotarajiwa kuanza muda wowote kuanzia sasa.

Naibu Kamishina wa Utalii na Huduma za Biashara wa Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapori Tanzania (Tawa), Imani Nkuwi, alisema hayo jana wakati akitolea ufafanuzi kuhusu uamuzi wa serikali kutaka Watanzania waanze kunufaika moja kwa moja na rasilimali za wanyamapori.

Alisema uamuzi huo ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli alilolitoa mwaka jana akiwa mkoani Katavi kuwa umefika wakati kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kuruhusu wananchi kuuza nyamapori ili kunufaika na rasilimali hiyo.

Nkuwi alisema ni wakati mwafaka kwa Watanzania kujitokeza na kuomba leseni za bucha za nyama kwa kuwa hali hiyo itawasaidia kujiongezea kipato na ajira.

Alisema tangu Rais Magufuli atangaze uamuzi huo, kumekuwa na hatua mbalimbali za kikanuni za uanzishwaji wa bucha za nyama za porini na kuwa mpaka sasa hatua iliyofikiwa ni nzuri.

# NDIDI HANA MPANGO KUONDOKA LEICESTER



**LONDON,** England

WILFRED Ndidi hana mpango wa kuondoka Leicester City licha ya uvumi kumhusisha na kutakiwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu ya England, huku raia huyo wa Nigeria akimshukuru kocha, Brendan Rodgers kwa kumsaidia kukuza kipaji chake.

Ndidi mwenye umri wa miaka 23, alijiunga na Leicester kutoka klabu ya nchini Ubelgiji ya Genk Januari mwaka 2017 na haraka akajiimarisha yeye mwenyewe kwenye kikosi cha kwanza kwa timu hiyo.

Amekuwa mmoja wa wachezaji wenye mchango mkubwa kwa Leicester ambao wamefurahia msimu wa 2019-20 kabla ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, huku wakiwa kwenye nafasi ya tatu kwenye msimamo.

Kiwango cha Ndidi kimeziibua klabu kadhaa kuwania saini yake, huku Manchester United wakitajwa kwamba wanavutiwa mno na mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria.

Hata hivyo, Ndidi hana mpango wa kuondoka haraka kwenye timu hiyo, huku mkataba wake wa sasa na Leicester ukitarajiwa kumalizika mwaka 2024.

"Tunafanya vizuri na ninafurahia kucheza hapa. Bado nina mkataba na Leicester," alisema akiiambia ESPN.

"Najifunza na najaribu kujiimarisha mimi mwenyewe kila siku, na nafanya vizuri hapa, hivyo kwa sasa sihitaji kwenda popote."

# Capello: Martinez usiende Barca

**MILAN,** Italia

NYOTA wa Inter Milan, Lautaro Martinez, anatakiwa kukataa uhamisho wa kwenda Barcelona kwani atakwenda 'kuozea' benchi kwa mabingwa hao wa LaLiga, kwa mujibu wa Fabio Capello.

Martinez ameripotiwa kuwa kipaumbele cha kwanza kwa Barca kwenye usajili wa kipindi cha majira ya joto, wakati miamba hao wa Hispania wakiangalia mtu wa kuziba pengo la muda mrefu la Luis Suarez.

Huku pia akiwa anahusishwa kutakiwa na Real Madrid na Manchester City, Martinez amefunga mabao 16 katika mechi 31 kwenye mashindano yote msimu huu kabla ya ligi kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Lakini kocha wa zamani wa Madrid, Milan na Juventus, Capello amemshauri mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina kubakia Inter.

"Kama ningekuwa mimi ningebakia Inter," alisema Capello akiliambia gazeti la La Gazzetta dello Sport.

"Pale Barcelona atasugua benchi."

Martinez ana kipengele kwenye mkataba wake cha kuachiwa cha pauni milioni 111 na Inter hawapo tayari kukubali chini ya kiasi hicho wakati Barca wakiongoza mbio za kuwania saini yake.





# Ronaldinho aendelea kusisitiza hana hatia

**ASUNCIO,** Paraguay

NYOTA wa zamani wa Brazil na Barcelona, Ronaldinho ameendelea kubainisha kwamba yeye hana makosa baada ya kuingia nchini Paraguay kwa hati ya kughushi.

Ronaldinho alisema kwamba, ilikuwa jambo la kushangaza kwake kuona kwamba hati hiyo ni ya kughushi kwa sababu yeye alijua ni halali na iliyokamilika.

Ronaldinho na Roberto Assis, ambaye ni kaka na wakala wake wa zamani, walikamatwa Machi 6, mwaka huu muda mfupi baada ya kuingia katika Jiji la Asuncion kwa ajili ya uzinduzi wa promosheni ya kitabu na casino ya mtandaoni.

Mamlaka ya nchini Paraguay walionyesha kitambulisho cha Ronaldinho kikiwa na picha yake, ambapo mshindi huyo wa zamani wa Ballon d'Or na kaka yake walipelekwa mahabusu.

Kwa muda wote, wawili hao walikuwa wakipaza sauti zao kuwa hawana kosa, lakini walikaa jela kwa siku 32 kabla ya kuachiwa kwa dhamana na kuwekwa kizuizini hotelini Aprili 8, mwaka huu.

Huku uchunguzi ukiwa unaendelea, Ronaldinho amefanya mahojiano yake ya kwanza tangu kukamatwa, akisisitiza hakujua kabisa kama hati hizo zilikuwa za kughushi.

"Kwa uhakika tulishangazwa kujua kwamba nyaraka zote hazikuwa halali," alisema Ronaldinho akikiambia kituo cha televisheni cha Paraguay, ABC Color.

# Lingard: Mwili mdogo umenipa shida United

**MANCHESTER,** England

JESSE Lingard amefunguka na kuelezea namna gani alivyopambana ili kuimarisha kiwango chake kwenye kikosi cha Manchester United.

Lingard alilazimika kusubiri ili kupata nafasi ya kuanza kucheza kwenye kikosi cha kwanza katika klabu hiyo aliyojiunga nayo miaka saba iliyopita, lakini tangu hapo amecheza mechi 202 kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya England.

Na sasa nyota huyo wa timu ya Taifa ya England amebainisha kwamba, namna gani nguvu na mwili mdogo ulivyompa wakati mgumu wa kuchomoza kwenye kikosi cha kwanza pale United.


"Mimi mwili wangu mdogo," alisema Lingard akinukuliwa na tovuti ya Manchester United.

"Wakati nilipokuwa kwenye timu ya vijana chini ya umri wa miaka 18, mara zote nilicheza timu ya vijana chini ya umri wa miaka 16 kwa sababu watu wengi walikuwa wakubwa kimwili kuliko mimi, lakini hilo halikunikatisha tamaa.

"Nilipambana na kujituma, mara zote nilitulia na kufanya vitu sahihi tu. Nafikiri ni jambo la kujituma tu, na kutuliza akili yako kwa kile unachokifanya, ingawa kuna wakati inakatisha tamaa.

"Nilikwenda kucheza kwa mkopo, kule pia nililazimika kupambana ili kupata nafasi nirudi tena United."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, hivi sasa amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka pale Old Trafford baada ya kushindwa kuwa kwenye kiwango cha kumshawishi kocha Ole Gunnar Solskjaer.



# KLOPP AFANANISHWA NA DALGLISH - ADAM



**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, anafanana na gwiji wa klabu hiyo, Kenny Dalglish, linapokuja suala la kujenga uhusiano mzuri na wachezaji, kwa mujibu wa Charlie Adam.

Kikosi cha Klopp kilikuwa na nafasi nzuri ya kutwaa taji la Ligi Kuu ya England kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 30 wakati msimu huo uliposimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Kocha huyo raia wa Ujerumani ameshuhudia maendelea mazuri zaidi kwa kikosi hicho tangu alipochukua mikoba ya kukinoa Oktoba mwaka 2015, akitwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kuwafunga Tottenham Hotspur kwenye fainali.

Kiungo wa zamani wa Liverpool, Adam, ameridhishwa na staili ya Klopp katika mahusiano yake na wachezaji na kumlinganisha na Dalglish, ambaye alikuwa kocha wakati kiungo huyo aliposajiliwa kwa 'Wekundu' hao.

"Wote wanaonekana kufanana sana, wapo wazi kwa wachezaji, wanawakumbatia wachezaji katika kila jambo," alisema Adam akinukuliwa na Sky Sport. "Sijawahi kufanya kazi na Jurgen, lakini kile ninachokiona kutoka nje, kwa hakika kabisa anaonyesha anafanya kazi ya kuvutia zaidi.

"Watu wanazungumza kuhusu klabu na namna alivyowaunganisha wachezaji wake, ni makocha wachache sana wenye uwezo huo. Yeye hana makuu na kila jambo anachukulia kwa mtazamo chanya."

# Chelsea haijajikita kumsajili Coutinho

**LONDON,** England

KLABU ya Chelsea inaaminika haijajikita vilivyo katika mpango wa kuwania kumsajili nyota wa Barcelona, Philippe Coutinho, kipindi kinachokuja cha majira ya joto, licha ya ripoti kutoka nchini Hispania kudai kwamba dili hilo linakaribia kukamilika.

'Blues' hao wanatakiwa kuimarisha safu yao ya ushambuliaji kipindi kinachokuja cha majira ya joto, kwani wote Willian na Pedro wanatarajia kuondoka wakati mikataba yao itakapomalizika mwishoni mwa msimu huu.

Na Coutinho ambaye anacheza pale Bayern Munich kwa mkopo ndiye anayetajwa kuwa kwenye rada za Chelsea.

Habari kutoka nchini Hispania zinadai kwamba, tayari makubaliano yameshafikiwa kuhusu usajili wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil.

Hata hivyo, gazeti la The Athletic limeripoti kwamba, kuna uwezekano mkubwa Chelsea wasikamilishe uhamisho huo.

Chelsea walikuwa wanamfuatilia Coutinho tangu akiwa na umri wa miaka 14 wakati akicheza nyumbani kwao nchini Brazil, wakati walipojaribu kutaka kumsajili.

Taarifa zaidi zinasema kwamba, ada yake ya kati ya pauni milioni 50 na milioni 70 inaonekana kuwa kubwa kwa Chelsea na hata mshahara wake wa pauni 225,000 kwa wiki nao wanaona watashindwa kuumudu.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AGUERO AMTETEA MESSI ARGENTINA

## Siwaelewi hao wanaomkosoa yeye katika timu ya taifa, ni wa kwanza kuteseka na...

**MANCHESTER,** England

SERGIO Aguero haelewi ukosoaji ulioelekezwa kwa Lionel Messi kwa Argentina, akisisitiza kwamba nyota huyo ndiye "wa kwanza kuteseka" na anaendelea kuwa tayari kuitumikia timu ya taifa.

**Messi ameshinda kila kitu katika muda wake akiwa pale Barcelona kama mchezaji – ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, LaLiga, UEFA Super Cup, Kombe la Klabu Bingwa Dunia, Kombe la Mfalme [Copa del Rey] na Super-copa de Espana.**

Hata hivyo, mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, bado hajaonja mafanikio akiwa na timu ya wakubwa ya Taifa ya Argentina baada ya kumaliza nafasi ya pili kwenye Kombe la Dunia 2014, pia amefanikiwa kufika fainali ya Copa America mara mbili mfululizo, mwaka 2015 na 2016.

Messi alijiondoa mwenyewe kwenye nafasi ya kuitwa timu ya taifa baada ya Argentina kutolewa katika hatua ya 16-bora ya Kombe la Dunia 2018, kabla ya kurejea na kuisaidia nchi yake kufika nusu fainali ya Copa America mwaka uliopita.

Mshambuliaji huyo, Messi mwenye umri wa miaka 32, ameendelea kukosolewa kwa kiwango chake Argentina, lakini raia mwenzake, Aguero amemtetea mchezaji mwenza huyo.

"Siwaelewi hao wanaomkosoa yeye katika timu ya taifa," Aguero aliiambi TyC Sports. "Ni wa kwanza kuteseka na kuendelea kuja."

Janga la virusi vya corona bado limesababisha michezo kusimama, huku Ligi Kuu England na LaLiga zikiwa miongoni mwa zilizoathirika, wakati michuano ya Copa America 2020 ikisogezwa mbele kwa mwaka ujao.

Ligi Kuu England iliahirishwa tangu mwezi uliopita na bado inabaki kusubiriwa kuona lini, na kama msimu wa 2019-20 utarejea.

Nyota wa Manchester City, Aguero ana mkataba hadi 2021 na mshambuliaji huyo wa Argentine amekuwa akihusishwa na kurejea katika klabu yake ya utotoni ya Independiente.

Lakini Aguero hajui ni vipi mustakabali wake wa baadaye utakavyokuwa, akiongeza: "Kwa sasa, sifiriki kuhusu nini cha kufanya. Na haya yote, klabu inayo matatizo.

"Hadi mwaka ujao inaweza kuongezwa kwa miezi miwili ama zaidi. Kuna wachezaji ambao wanamaliza mikataba yao mwaka huu na kama watachezeshwa Julai, Agosti ama Septemba, klabu itapata matatizo.

"Sijui kama wanaweza kuongeza mikataba na wachezaji kwa miezi mitatu ama sita. Jambo la kwanza ni kumaliza msimu huu na kugonga kila kitu kijacho. "

## ZISIKUPITE

### AUBAMEYANG KUPATA MRITHI

ARSENAL imekuwa ikipewa nafasi ndogo ya kumsajili winga wa Chelsea, Willian kwa ajili ya kuziba nafasi ya nahodha Pierre-Emerick Aubameyang. ***(The Sun)***

### COUTINHO, DEMBELE SOKONI

BARCELONA imewageuza chambo sokoni Philippe Coutinho na Ousmane Dembele tayari kwa ajili ya kubadilishana kwa mchezaji watakayetaka kumsajili. ***(Daily Mail)***

### CHELSEA YAMGEUKIA HAVERTZ

CHELSEA imegeuzia mitego yake kwa kiungo wa Bayer Leverkusen, Kai Havertz baada ya kumpotezea Philippe Coutinho. ***(Daily Star)***

### NEWCASTLE YAMTAKA BORINI

NEWCASTLE inatazama uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Sunderland, Fabio Borini, kwa mujibu wa taarifa kutoka Italia. ***(The Sun)***

### RICE NDANI RADA CHELSEA

TAARIFA za ndani za West Ham zimeeleza "hakuna yeyote aliye salama" katika klabu hiyo kutokana na kutaka kufanya mabadiliko makubwa ya kikosi majira haya ya joto na Chelsea ikitarajiwa kutoa takriban pauni milioni 70 kwa kiungo Muingereza Declan Rice, ambaye aliondoka 'Blues' akiwa na miaka 15. ***(The Sun)***

### LIVER, CITY KUMKOSA WHITE

LIVERPOOL, Manchester United na Manchester City zimeripotiwa kufungiwa katika mbio za kumsajili beki wa kati anayecheza kwa mkopo Leeds United, Ben White, akitokea Brighton & Hove Albion. ***(Daily Mirror)***

### EVERTON KWA KINDA BARCA

EVERTON imefanya mazungumzo na Barcelona kuhusu uwezekano wa kumpata beki kinda wa kati, Jean-Clair Todibo, anayeelezwa kuwa na thamani ya pauni milioni 17.4.***(Daily Mail)***

### FEDERICO AWINDWA UNITED

MANCHESTER United kwa sasa ni sehemu ya "klabu nne zinazopiga mbio" za kumsajili winga wa Fiorentina, Federico Chiesa. ***(Daily Star).***

### KEAN KUTIMKIA NAPOLI

MSHAMBULIAJI wa Everton, Moise Kean, 20, amekuwa akihusishwa na kujiunga na Napoli. Mtaliano huyo anaweza kuathibiwa na Everton baada ya kuvunja maelekezo ya serikali ya kujikinga na virusi vya corona mapema wiki hii. ***(Corriere dello Sport - in Italian)***

### YAJITOSA KWA PARTEY

ARSENAL imetoa ofa ya pauni milioni 43 kwa kiungo wa Atletico Madrid na Ghana, Thomas Partey, 26. ***(Express)***

### SPURS, EVERTON VITANI

TOTTENHAM, Everton na Southampton ni miongoni mwa klabu ngeni zilizotuma mashushushu wao kwenda kumtazama beki wa Strasbourg, Mohamed Simakan. ***(RMC Sport)***

HABARI MICHEZO

## JKT Tanzania lengo kuishusha Coastal Union

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuzidiwa kwa pointi nne na Coastal Union iliyopo katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara, uongozi wa timu ya JKT Tanzania, umepania kuishusha miamba hiyo ya Tanga kwa kumaliza katika nafasi hiyo msimu huu.

Hadi Ligi Kuu inasimama Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, JKT Tanzania ipo nafasi ya saba ikiwa na alama 42 baada ya mechi 28, nyuma ya Polisi Tanzania inayoizidi kwa alama tatu lakini ikiwa mbele kwa mchezo mmoja, huku Coastal yenye pointi 46 ikicheza mechi sawa na 'Wanajeshi' hao.

Akizungumza na Nipashe jana, Makamu Mwenyekiti wa timu hiyo, Thabit Baraji, alisema ingawa bado hawajajua hatma ya ligi hiyo kurejea, malengo yao ni kumaliza katika nafasi tano za juu.

Alisema tayari wamewaeleza makocha kuwahimiza wachezaji wao kufuata ipasavyo mazoezi binafsi ili kuhakikisha wanaporejea katika ligi wanakuwa bora na kufikia malengo hayo.

"Malengo yetu tumalize ligi katika nafasi ya tano, tumewaeleza makocha kwamba wazungumze na wachezaji wetu kujituma katika kipindi hiki cha mapumziko ya corona ili watakaporejea wesiwe na kazi kubwa," alisema Thabit.

Alisema mechi zilizobakia kwa sasa ni ngumu hasa kwa upande wa timu zilizopo kati kutokana na waliopo mwishoni mwa msimamo kupambana kutafuta alama zitakazowanusuru kushuka daraja.

## Wachezaji Mwadui wawekwa sokoni

**Na Shufaa Lyimo**

KUELEKEA dirisha kubwa lijalo la usajili Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Klabu ya Mwadui FC, Khaleed Adam, amewaweka wachezaji wake wote sokoni baada ya kueleza endapo timu yoyote itajitokeza kumhitaji mchezaji wake, yupo tayari kumuachia kwa kuwa ni "mpenda maendeleo".

Akizungumza na Nipashe jana, Khaleed alisema endapo watakubaliana kimaslahi hatakuwa na sababu ya kumzuia mchezaji.

"Kama mchezaji wangu atapata nafasi ya kuhitajika na timu nyingine, nitamruhusu kwa sababu napenda wachezaji wangu wapate maendeleo," alisema Khaleed.

Alisema anafahamu mchezaji akitoka sehemu moja kwenda nyingine anapata mafanikio ambayo yatamsaidia kuendeleza soka na familia yake.

Kuhusu maendeleo ya wachezaji wake alikiri kuendelea vizuri na kusema wapo makini na programu aliyowapa katika kipindi hiki ambacho Ligi Kuu imesimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

# DAS MUHEZA, BABU SEYA WAACHIA SINGO YA CORONA

**Na Steven William,** MUHEZA

WAKATI kimya kingi kikitanda kwa wasanii baada ya shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko kuzuiwa na serikali ikiwamo matamasha ya muziki, kutokana na mlipuko wa maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19), mke wa Nguza Viking 'Babu Seya', Desderia Haule, amewaamsha kwa kutunga 'mpini' mkali wa corona.

**Desderia ambaye ni Katibu Tawala (DAS) wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, amejitosa katika fani ya usanii wa muziki na hatimaye kuibuka na singo ya wimbo wenye ujumbe wa ugonjwa hatari wa corona.**

Nyimbo hiyo ambayo imebeba jina la albamu "Mungu Tusamehe", tayari imekamilika na kuanza kurushwa katika mitandao mbalimbali ya kijamii pamoja redio za nchini.

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Haule alisema nyimbo hiyo wameirekodi kwa kushirikiana na mumewe Babu Seya, ambaye ni miongoni mwa wanamuziki wenye jina kubwa katika tasnia hiyo ndani na nje ya nchi.

Alisema ametunga wimbo huo wa corona ili kuomba msamaha kwa Mungu ashushe baraka zake za uponyaji na kulipeperusha janga hilo ambalo hadi jana mchana jumla ya watu 3,082,726 duniani kote walishathibitika kuwa na maambukizo ya virusi hivyo huku walipoteza maisha wakiwa 212,486.

Aidha, Haule alisema wimbo huo pia ni maalum kwa ajili ya kumuunga mkono Rais John Magufuli katika juhudi zake za kuhimiza Watanzania kuliombea Taifa kwa Mungu ili aiepushe Tanzania na janga hilo linaloitesa dunia kwa sasa.

Kwa upande wa mumewe, Babu Seya, alisema katika wimbo huo ameingiza sauti yake na kusaidia kupiga vyombo kwa ajili ya kumuunga mkono mkewe katika wimbo huo wa corona.

Alisema kwa sasa wimbo huo umeanza kuvuma katika mitandao ya kijamii na wanajiandaa kupeleka katika vituo vya televisheni nchini ili kutambulika singo ya ujumbe wa corona.

Babu Seya alisema kutokana na serikali kuzuia mikusanyiko, wamepanga kuuzindua rasmi pindi hali itakapokuwa shwari, lakini utaendelea kupigwa na katika vituo vya redio na televisheni.

Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Mhandisi Mwanasha Tumbo, akizungumzia wimbo huo, alisema umekuwa ni chachu katika kuunga mkono juhudi za kutoa elimu kwa wananchi kujikinga na corona.



Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, Desderia Haule, ambaye ameachia singo ya corona akiwa na mumewe, Nguza Viking maarufu Babu Seya.
**PICHA: STEVEN WILLIAM**

## *Ajibu agawa msaada janga corona*

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa Simba, Ibrahim Ajibu, amekuwa mchezaji wa kwanza nchini kutoa msaada binafsi kwa wahitaji katika kipindi hiki ambacho dunia inakabiliwa na janga la ugonjwa wa COVID-19, unaosababishwa na virusi ya corona.

Juzi, Ajibu alitoa msada kwa watoto yatima kwenye Kituo cha Umra kilichopo Magomeni Mikumi na Mayunga kilichopo Kinondoni Moscow, vyote vya jijini Dar es Salaam.

"Mimi Ajibu mchezaji wa Simba, kama Mtanzania, nimeguswa sana na janga lililotukabili kwenye nchini yetu na dunia kwa jumla la ugonjwa wa corona. Nimeamua kuanzisha kampeni hii ya kuisaidia jamii na watoto yatima, kwenye kampeni hii ya kujitolea, vifaa kama sanitizer [vitakasa mikono], ndoo za kunawia mikono, pamoja na chakula," alisema na kuongeza.

"Pia ningependa kutoa hamasa kwa wadau wengine ili kujiunge na mimi kufanikisha zoezi hizi."

Ajibu alisema kuwa hiyo si mara ya kwanza kwake kugawa misaada kwa watoto yatima, kwani ni sehemu ya maisha yake kufanya hivyo mara kadhaa.

"Nitakuwa nikiendelea kutoa kadri Mungu atakavyokuwa ananijaalia, nitakuwa nagawana na watoto yatima, kutegemeana na kipato changu," alisema.

Kujitolea kwa mchezaji huyo kumezua mjadala mkubwa mitaani kwa wadau wa soka kuwataka baadhi ya wachezaji wa Kitanzania vipenzi vya mashabiki kuiga mfano wake huku pia klabu kongwe nchini Simba na Yanga zikitakiwa kutobaki nyuma katika kipindi hiki kigumu ambacho taifa linakabiliwa na janga hilo la corona.

Kwa upande wa klabu ya Simba Ajibu ni mchezaji wa pili kufanya hivyo, baada ya Mkenya Francis Kahata kugawa lita 10,000 za maji kwa jamii inayomzunguka nyumbani kwao jijini Nairobi wakati huu wa janga la corona.

Michezo
Jumatano Aprili 29, 2020
Nipashe




Aguero amtetea Messi Argentina UKURASA 22

WATANO...




Rais wa Shirikisho la Soka duniani (Fifa), Gianni Infantino, ambaye jopo lake limependekeza kuongezwa kwa wachezaji watano wanaotokea benchi 'sab' wakati ligi zitakaporejea. **PICHA: MTANDAO**

# FIFA YAITAKA TFF KUTUMIA 'SAB' 5

## ●●● Yaunga mkono pendekezo la kocha wa Azam FC la wachezaji wa kutokea benchi...

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU chache baada ya Kocha Mkuu wa Azam FC, Mromania Aristica Cioaba, kulitaka Shirikisho la Soka nchini (TFF) pamoja na Bodi ya Ligi (TPLB), kuangalia uwezekano wa Ligi Kuu itakaporejea kuruhusu timu kufanya mabadiliko 'sab' (substitutions) tano badala ya tatu, Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), limeungana naye katika hoja hiyo.

**Akitoa hoja hiyo wiki iliyopita, Cioaba alisema ni vema TFF na TPLB zikaangalia uwezekano wa kubadili kanuni na kuruhusu mabadiliko matano katika mechi moja ili kuwaepusha wachezaji na kukumbwa na majeraha kutokana na kuwa nje ya uwanja bila kucheza mechi kwa muda mrefu.**

Kauli hiyo iliungwa mkono na Fifa juzi baada ya kupendekeza kwamba timu zitaruhusiwa kufanya mabadiliko ya wachezaji watano kwa kila mchezo kutokana na ratiba kubana wakati mashindano mbalimbali yatakaporejea tena baada ya janga la corona kupita.

Janga la virusi vya corona limesabisha ligi nyingi duniani kusimama ikiwa ni pamoja na Ligi Kuu Bara, huku ile ya Uholanzi 'Eredivisie' ikiwa ni miongoni mwa zilizofutwa kabisa.

Timu zinakabiliwa na rundo la upangwaji wa ratiba ngumu mwishoni wakati zitakaporejea na Fifa inatumai kupunguza mzigo mkubwa kwa wachezaji kwa kuruhusu nyongeza ya 'sab' mbili kutoka tatu za awali, wakati wa mechi ama jumla ya mabadiliko kuwa sita kama mechi itakwenda muda wa nyongeza.

Chombo hicho chenye dhamana ya soko duniani, kitakuwa na chaguo la kuingiza sheria hiyo mpya ya muda hadi mwishoni mwa msimu, wakati pia itatumika kwa mechi za timu ya taifa hadi za Desemba 31, mwakani.

Msemaji wa Fifa alisema: "Wakati mashindano yatakaporejea, mashindano kama haya yanaweza kukabiliwa na mrundikano uliotokana na kalenda kubana visivyo kawaida kwa mechi kuchezwa katika wiki mfululizo.

"Usalama wa wachezaji ni moja ya kipaumbele muhimu kwa Fifa. Wasiwasi mmojawapo katika suala hili ni kwamba mzunguko wa juu zaidi kuliko wa kawaida unaweza kuongeza hatari ya majeruhi yanayoweza kutokea kutokana na wachezaji kubebeshwa mzigo mkubwa.

"Kwa kuzingatia hii na kwa kuzingatia changamoto ya kipekee inayoikabili dunia katika kufanikisha mashindano kulingana na kalenda iliyotabiriwa hapo awali, Fifa inapendekeza idadi kubwa ya wachezaji kufanyiwa mabadiliko kuruhusiwa kwa muda kwa hiari ya waandaaji wa mashindano husika.

# Wachezaji Simba 'mizani' wakirejea

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa klabu ya Simba wanatarajiwa kupimwa ili kujua kama walikuwa wanafanya mazoezi binafsi au la kutokana na michezo kusimama kupisha kuepuka ugonjwa wa COVID-19, unaosababishwa na virusi vya corona.

Meneja wa klabu hiyo, Patrick Rweyemamu (pichani) alisema jijini Dar es Salaam juzi kuwa mara mazoezi yatakapoanza, wachezaji wote wa klabu hiyo watapimwa ili kujua kama walikuwa wanafuata maagizo ya Kocha Mkuu, Mbelgiji Sven Vandenbroeck ya kufanya mazoezi binafsi wakiwa majumbani ama la.

"Tukikutana tunafanya testi ili kujua kama wachezaji walikuwa wanafanya mazoezi, na walikuwa wanafanya kwa kiwango gani," Rweyemamu alisema.

"Tunafuatilia kwenye mitandao mazoezi yao kwa sababu wanatutumia, lakini sisi tumejiwekea masharti kuwa mazoezi rasmi yatakapoanza itabidi tujiridhishe."



Ligi Tanzania Bara ilisimama rasmi Machi 17, mwaka huu, baada ya agizo la serikali la kusitisha shughuli zote zinazosababisha mikusanyiko ya watu ikiwamo michezo kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona ambavyo hadi kufikia jana mchana jumla ya watu 3,082,726 duniani kote walishathibitika kuwa na maambukizo huku waliopoteza maisha wakiwa 212,486.

Hadi Ligi Kuu inasimama, Simba ilikuwa inaongozwa ligi ikiwa na pointi 71, ikifuatia na Azam FC yenye alama 54 na Yanga 51 lakini ikiwa nyuma kwa mchezo mmoja.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >